KUCHUNGUZA DHIMA ZA NYIMBO ZA ASILI ZA WATOTO ZA WAHEHE

ANNA MICHAEL MLAMBIA

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii yenye mada **"*Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Asili za Watoto za Wahehe*"** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya digrii ya M.A (Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

_____

Dkt Mohamed Omary

(Msimamizi)

_____

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kumiliki kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi **Mlambia Anna Michael**, natamka hapa na kuthibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa na wala haitahudhurishwa popote pale katika Chuo Kikuu chochote kwa lengo la kufuzu na kutunukiwa shahada kama hii.

_____

Sahihi

_____

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu na familia yangu na pia kwa wote wenye mapenzi na lugha ya Kiswahili.

SHUKRANI

Mungu Mwenyezi mwingi wa rehema ninakushukuru kwa yote uliyonijalia. Natambua uwepo wangu hapa duniani na uzima nilionao ni kwa ajili ya Mungu baba. Ninakushukuru Mungu baba kwa kunipa afya, kunilinda, kunipa akili na uwezo wa kupembua mambo. Wapo waliotamani kuvipata vyote hivi lakini hawakufanikiwa umeninusuru na kifo bado naendelea kuishi kwa neema yako asante sana Mungu Baba. Pia umeibariki kazi yangu hii ya utafiti nimeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Nimeweza kuikamilisha kazi hii kwa kupitia michango ya mawazo ya watu mbalimbali ambao wameshirikiana nami bega kwa bega ili kuhakikisha inafanyika na kukamilika kama ilivyopangwa. Ninachukua nafasi hii ya pekee kutoa shukrani zangu za dhati kwao. Kwa kuwa watu walionipa ushirikiano kwa namna moja au nyingine ni wengi ni vigumu kuwataja wote. Ila itanilazimu kuwataja wachache kwa niaba ya wote walioshiriki na kuniwezesha kwenye kazi hii. Nikianza na Dkt Hadija Jilala aliyenifundisha mbinu za utafiti akishirikiana na Prof. E. Mbogo na Prof. T. Sengo. Shukrani nyingi ziwafikie.

Pia, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwalimu wangu Dkt Omary Mohamed ambaye ndiye msimamizi wangu katika utafiti huu, amenifundisha, amenielekeza, ameniongoza, amenikosoa mara nyingi ninamshukuru kwa kunivumilia hata pale aliponirekebisha aliweza kutumia gharama zake na kupoteza muda wake siku za mapumziko, ameweza kunitia moyo katika kazi hii. Ukweli moyo wake wa kunijali na kunithamini naomba Mungu ambariki afya njema naye afanikwe zaidi katika

maisha yake na familia yake. Vile vile natoa shukrani za dhati kwa mwalimu wangu Nasra Habiba kwa mchango wako mkubwa wa hali na mali katika kunishauri na kunipa moyo wa kuendelea na utafiti huu.

Kwa namna ya pekee ninatoa shukrani za dhati kwa Mwalimu Mpeli Mwankusye kwa mchango wake mkubwa uliofanikisha pendekezo la utafiti na mchango wake mkubwa uliofanikisha ukusanyaji wa data. Pia amenisaidia sana kuniongoza katika kuhakikisha nafikia malengo ya kazi hii. Mungu ambarikie moyo huo wa upendo kwa wengine, hana wivu kwa kile anachokijua anakuelekeza.

Nawashukuru marafiki zangu mwalimu A. Kiyeyeu, Madina Mfilinge na Joyce Amon kwa kunisaidia kukusanya data. Pamoja na wanafunzi wa shule za msingi Tumaini na Mwaya kwa kunikusanyia data.

Shukrani zangu za dhati zimwendee mume wangu Col. Fidelis A. Mnyanyi (Mstaafu) bila kinyongo kuniruhusu na kunivumilia kwa yote yaliyojitokeza na kunipa ushirikiano wa hali na mali na kuniwezesha mahitaji mbalimbali. Pamoja naye wanetu Irene na Jackson kwa uvumilivu wao wa kukosa mapenzi ya mama na kukosa mahitaji yao ya msingi kipindi chote cha masomo, bila kumsahau mdogo wangu mpendwa Delphina Mlambia kwa mchango wake kuniwezesha kwa kila hitaji, alijinyima hata kuwanyima wanae ili anifanikishie mahitaji yangu. Michango yenu kwangu sitoisahau kamwe kwa namna ya pekee niwashukuru wazazi wangu walionileta hapa duniani Elizabeth Chelula na Michael Mlambia. Ingawa Mungu aliwapenda zaidi. Mama alinitoka ghafla nikiwa ndani ya hii kozi pia alinivumilia sana hata pale alipohitaji msaada wangu. Kaka yangu mpendwa Richard Mlambia

ninakushukuru kwa yote uliyonisaidia ingawa nawe umetangulia mbele ya haki nikiwa kwenye harakati za utafiti, wadogo zangu Suzana na Inocenti mmeniachia majukumu ya kulea watoto wenu sikuwa karibu nao kipindi chote cha kozi yangu nao wamenivumilia niwashukuru pia.

Nitakuwa si mwingi wa fadhila kutomshukuru mkuu wangu wa kazi Secilia Muyinga kwani amenipa ushirikiano wa pekee pale aliponiruhusu baada ya kumaliza kufundisha vipindi vyangu na kwenda kukusanya data nakushukuru sana bila wewe zoezi hili lingekwama.

Pamoja na wote hao napenda kumshukuru rafiki yangu na mdogo wangu Martha Silavwe ambaye tumekuwa naye bega kwa bega kwenye kozi hii kwa kutiana moyo na wanafunzi wenzangu wa ma-kiswahili kwa mchango wa mawazo yaliyosaidia utafiti huu.

Mwisho kabisa nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wale wote waliotoa mchango wao hata kuwezesha utafiti huu kufanikiwa mwaka huu bila kumsahau mchapishaji wa utafiti huu Nuru Allan wa Gwivaha Enterprises Company.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni Kuchunguza dhima za nyimbo za asili za watoto za Wahehe. Mada hii ya utafiti ilikuwa na malengo mahususi mawili ambayo yalikuwa ni kuchambua dhima za nyimbo za asili za watoto za Wahehe wa mkoani Iringa na kubainisha nafasi ya nyimbo za asili za watoto za Wahehe katika jamii hiyo. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za ushuhudiaji, usaili na hojaji na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia za Uamilifu, Uasilia na Uhalisia. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa nyimbo za asili za watoto za Wahehe zina dhima muhimu katika jamii hiyo. Dhima hizo ni pamoja na Kuhamasisha maadili mema, kuonya jamii, kuelimisha jamii, kuchapulisha kazi, kutunza mila na desturi, Kupiga vita uchawi, kuagana na wazazi na kudumisha heshima katika jamii. Dhima hizi zina nafasi kubwa katika kuifanya jamii ya Wahehe kuwa yenye umoja na mshikamano katika maisha yao ya kila siku.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKRANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **ix**

ORODHA YA MAJEDWALI ..... **xiv**

SURA YA KWANZA **1**

1.0 UTANGULIZI **1**

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Tatizo 1

1.3 Tatizo la Utafiti 6

1.4 Malengo ya Utafiti 7

1.4.1 Lengo Kuu 7

1.4.2 Malengo Mahususi 7

1.5 Maswali ya Utafiti 7

1.6 Umuhimu wa Utafiti 7

1.7 Mipaka ya Utafiti 8

1.8 Mpangilio wa Tasnifu 9

SURA YA PILI **10**

2.0 MAPITIO YA MACHAPISHO NA MKABALA WA KINADHARIA **10**

2.1 Utangulizi 10

2.2 Dhana ya Nyimbo kwa Ujumla 10

2.2.1 Nyimbo Kama Kipengele cha Fasihi na Kazi Zake 10

2.2.2 Nyimbo za Asili kwa Ujumla na Nyimbo za Watoto 12

2.3 Aina za Nyimbo za Asili za Watoto..... 13

2.4 Dhima za Nyimbo 13

2.4.1 Dhima za Nyimbo za Asili kwa Ujumla 14

2.4.2 Dhima katika Nyimbo za Asili za Watoto 14

2.5 Nafasi ya Dhima za Nyimbo za Asili za Watoto kwa Jamii 15

2.6 Pengo la Utafiti 17

2.7 Kiunzi cha Nadharia..... 18

2.7.1 Nadharia ya Uamilifu..... 19

2.7.2 Nadharia ya Uasilia..... 20

2.7.3 Nadharia ya Uhalisia..... 21

2.8 Hitimisho..... 22

SURA YA TATU 23

3.0 MBINU ZA UTAFITI..... 23

3.1 Utangulizi..... 23

3.2 Muundo wa Utafiti 23

3.3 Eneo la Utafiti 24

3.4 Aina ya Utafiti..... 24

3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa 24

3.5.1 Data za Msingi 24

3.6 Mbinu za Kukusanya Data..... 25

3.6.1 Ushuhudiaji 25

3.6.2 Usaili 25

3.6.3 Hojaji 26
3.7 Sampuli na Usampulishaji 27
3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data 28
3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo 29
3.9 Maadili ya Utafiti 29
3.10 Hitimisho 29
SURA YA NNE 31
4.0 UCHAMBUZI WA DATA 31
4.1 Utangulizi 31
4.2 Dhima katika Nyimbo za Asili za Watoto za Wahehe 31
4.2.1 Kuhamasisha Maadili Mema 32
4.2.2 Kuonya Jamii 35
4.2.3 Kuelimisha Jamii 37
4.2.4 Kuchapulisha Kazi 42
4.2.5 Kutunza Mila na Desturi 46
4.2.6 Kupiga Vita Uchawi 48
4.2.7 Kuagana na Wazazi 49
4.2.8 Kudumisha Heshima 50
4.3 Hitimisho 52
SURA YA TANO 54
5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO 54
5.1 Utangulizi 54
5.2 Hitimisho 54
5.3 Muhtasari 54

5.4 Mapendekezo 55

MAREJEO 57

VIAMBATISHO 59

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Utafiti Katika Jedwali 28

Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Watafitiwa Wanaokumbuka Nyimbo..... 31

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii ni ya utangulizi wa utafiti unaolenga kuchunguza dhamira katika nyimbo za asili za watoto katika mkoa wa Iringa. Sura hii inahusisha vitu vifuatavyo: Usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti (lengo kuu na malengo mahususi), maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti, mpangilio wa tasinifu na hitimisho.

1.2 Usuli wa Tatizo

Jamii ya Kiafrika ina utajiri mkubwa sana wa nyimbo katika michezo ya watoto. Zipo nyimbo za kiasili na pia nyimbo za kisasa ambazo watoto huimba wakiwa wanacheza michezo yao ya kitoto. Nyimbo za asili ni nyimbo za zamani za makabila, na nyimbo za kisasa ni nyimbo wanazoimba siku hizi ambazo zina mchanganyiko wa jamii tofauti zina mitindo toka mataifa ya nje kama bongo fleva. Nyimbo za asili za watoto zilikuwa ni darasa tosha kwa watoto. Hivyo basi utamaduni wetu hapa Tanzania nao ni tajiri, katika nyimbo za watoto. Nyimbo nyingi zina mafundisho ndani yake na zina maneno yenye maana ya kufanya mwenendo wa watoto uwe mzuri na kwa kuwafanya watoto wasipende kufanya mambo yasiyokubalika na jamii zao. Kupitia nyimbo, watoto huweza kujifunza tabia njema hata bila kuwapa adhabu yoyote ile. Watoto hupenda kuimba nyimbo kwa kuwa zinafurahisha.

Pia nyimbo hizo wanazoziimba huwa na maneno ambayo yanawaingia akilini mwao,

na taratibu huwapelekea kuelekea kufuata mwenendo ule unaopendekezwa na nyimbo waziimbazo (Thonya, 1979).

Balisidya (1989) anaelezea kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zinazotumia melodia, mahadhi, kongosie na mapigo. Mgeni (2014) anajaribu kueleza kuwa nyimbo ni kipengele muhimu sana katika jamii zote ulimwenguni. Ni utanzu uliothaminiwa sana enzi hizo.

Wataalamu na watafiti mbalimbali wa fasihi simulizi wameweza kuelezea asili ya nyimbo. Sengo (1978) na Finnegan (1977) katika kuelezea asili ya nyimbo walieleza kuwa nyimbo zilianza pale tu binadamu alipoanza kupambana dhidi ya mazingira yake katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Senkoro (1987) amechunguza na kuona kuwa chimbuko la nyimbo ilikuwa ni kazi, mfano wimbo uliimbwa kumpa mtu ari na nguvu ya kufanya kazi. Pia wimbo ulikuwa na nguvu za kiuchawi zilimfanya mtu asahau uchovu na asijali jasho jingi mwilini wala jua kali angani na wimbo uliotumika kuwahamasisha wanajamii kuungana na kufanya kazi pamoja (Senkoro, 1987). Katika kuelezea sintofahamu juu ya asili ya nyimbo na muziki Mgeni (2014) anamnukuu Schumann (1994) anadai kuwa “muziki na nyimbo ni yatima ambaye wazazi wake hawajulikani kamwe. Hata hivyo mbali na nukuu hiyo juu ya utata wa uasili wa nyimbo bado muziki na nyimbo vimeendelea kuonekana kuwa vitu bora zaidi katika jamii (Mgeni, 2014).”

Katika kujaribu kuainisha aina mbalimbali za nyimbo Mazingwa (1991), Ngure (2003) na Nkwera (1998) wametazama zaidi nyimbo zilizoimbwa katika sherehe

kama vile harusi na kumtoa mwari. Mazingwa (1991) naye aliangalia zaidi dhamira za nyimbo katika makabila ya Wazaramo na Waruguru. Ngure (2003) anaendelea kueleza kuwa nyimbo za harusi ziliimbwa kwa furaha zikiashiria binti au kijana kupata jiko lakini pia nyimbo ziliweza kuimbwa kwa huzuni kuelezea masikitiko ya kuondoka kwa binti pale alipopazoea na kwenda asipopazoea sambamba na aina mbalimbali za nyimbo katika jamii yoyote ile kuna ushahidi wa kutosha juu ya upana wa dhamira za nyimbo katika jamii husika kuthibitisha hili. Mazrui (1986) katika mgeni wetu (2013) anabainisha kuwa, nyimbo kama kipera katika fasihi zina wajibu wa kumfanya mtu aitambue nafasi yake katika jamii na vile vile kutambua wajibu na majukumu yake. Mgeni (2014) akimnukuu Akuno (1999) anayesema nyimbo au muziki ukiwa na amali na kiunjozi kama kiburudisho, muziki huendeleza uhusiano wa mtu binafsi, hustarehesha na kumwezesha mtu kuwasilisha hisia zake. Pia nyimbo husaidia kuendeleza uhusuano wa kimazingira. Katika kuelezea dhamira za nyimbo, Mulokozi (1996) anasema nyimbo hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kuomboleza, kubembeleza mtoto anapolala, kuchapua kazi, kutoa hamasa vitani. Lakini Mulokozi alitazama katika kila muktadha unafungamana na wimbo huo na nafasi ya maudhui ya nyimbo hizo kwa hadhira.

Senkuli na Miruka (1990) katika Mulokozi (1996) wao wamejaribu kuelezea kuhusu nyimbo za jandoni (nyiso) kuwa kusudi la nyimbo hizo ni kuwaasa wari kuhusu majukumu yao mapya ya utu uzima. Kuwaandaa wari kihisia, kuyakabili maumivu ya kimwili (kama tohara, kutolewa bikra) watakayoyapata katika kuuaga utoto na kusisitiza dhiki ya kiutu uzima inayowakabili wari.

Mulokozi (1996) aliziweka nyimbo katika makundi makuu manne ambayo ni tumbuizo, tukuzo, chapuzo na tendi au tenzi. Naye Balisidya (1989) ametafiti aina za nyimbo na kuzianisha kama vile: bembea, tahlili, tumbuizo, nyimbo za ngoma, miviga nyimbo za michezo na za siasa. Mbali na aina hizo zilizotajwa pia mtafiti Maeda (2016). Kwa upande mwingine, amezitaja aina zifuatazo za nyimbo; kiongozi (nyimbo za kuaga mwaka), nyimbo za dini, wawe (nyimbo zihusuzo kilimo), kimani (nyimbo zinazohusu shughuli za baharini), nyimbo za vita na nyimbo za uwindaji.

Nyimbo za watoto ziliimbwa kwa wakati tofauti. Zipo nyimbo walizoziimba wakati wa masika na wakati wa kiangazi. Kwa kuwa nyimbo zao ziliambatana na michezo, basi wakati wa masika walipendelea michezo ya kudaka (mdako) na kiboleni kwa kuwa ardhi ilikuwa ni chepe kwa sababu ya mvua (Thonya, 1979). Wapo watalaamu mbalimbali waliofanya utafiti wa nyimbo za watoto miongoni mwao ni Mulokozi (1989) yeye alijaribu kuzielezea nyimbo za watoto zilizoimbwa wakati wa michezo ya watoto wahusika wakiwa ni watoto wenyewe. Mwanza (2007) yeye alichunguza mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Katika kutazama dhamira za nyimbo za watoto Mbarouk (1983) alibaini kuwa nyimbo za watoto zilisaidia kunogesha michezo yao. Mgeni (2014) akimnukuu Akuno (1999) anaendelea kukazia kuwa nyimbo za watoto humfanya mtoto kuwa na umbo linalotarajiwa na jamii.

Katika kitabu cha *Mtoto, Michezo na Nyimbo*, Thonya (1979) alichunguza na kuelezea jinsi ya kucheza na kuimba nyimbo za watoto, akieleza pia manufaa ya michezo na nyimbo hizo na matumizi yake. Kwa ushahidi wa rejea nyingi hapo juu

ni dhahiri kuwa kazi nyingi zilizofanywa katika kuchunguza nyimbo za watoto, zimejikita katika kuangalia mtindo, pamoja na mifano hiyo ya nyimbo.

Aina ya pili ya michezo anasema ni ile yenye utaratibu maalumu ambayo inahitaji kufundishwa. Pamoja na kuwepo kwa waandishi na wataalamu wanaoelezea dhamira za nyimbo wamejaribu kuchunguza dhamira za nyimbo husika kwa ujumla wake bila kuangalia na kuchunguza dhamira za nyimbo za watoto hasa nyimbo za asili za makabila yetu katika mikoa mbalimbali ukiwemo mkoa wa Iringa ambako utafiti huu utafanyika. Kutokana na mwingiliano mkubwa wa tamaduni katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa mwingiliano umechangiwa na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kama alivyosema Maeda (2016) mwingiliano huo umesababisha upuuzwaji wa nyimbo za asili.

Utafiti huu umejikita kuangalia nafasi ya dhima ya nyimbo za asili za watoto katika mkoa wa Iringa. Utafiti huu pia uliangalia kwa kina dhima zilizotumika kuwaadilisha watoto na kuwafanya kutokwenda kinyume na mila na desturi zao. Hili litaenda sambamba na watoto kuthamini nyimbo hizo kama sehemu yao ya kuwaadilisha na kutunza utamaduni wao utambuzi wa nyimbo zenyewe kupitia utafiti huu utawasaidia watoto kutilia mkazo na kuheshimu mawazo yanayopatikana katika nyimbo hizo na itasaidia kutazama namna nyimbo hizo zinavyofaa katika jamii, ili kama kuna mapungufu yaweze kurekebishwa. Pia kwa kuangaza upungufu na uchanya katika maudhui yake. Hii ndiyo sababu ya kufanya utafiti huu.

Wahehe ni kabila ambalo linalopatikana mkoani Iringa. Mkoa wa Iringa una wilaya nne, ambazo ni pamoja na Iringa vijijini, Iringa Manispaa, Mufindi na Kilolo.

Wahehe wapo katika kila wilaya tajwa hapo. Katika mkoa wa Iringa kuna lahaja zifuatazo; Vadongwe, Vanafiwa, Vasagala, Vasangu Vasavila na Vanyakilwa. Kabila la Wahehe ni miongoni mwa makabila maarufu nchini, kabila hili halipo nyuma katika suala zima la kuenzi mila nyingi na desturi zake, ingawa baadhi ya mila zimeanza kupotea kutokana na usasa ikiwemo mambo ya utandawazi. Isitoshe mila hizo hazijaandikwa kiupana na wala hazikuhifadhiwa.

Kivenule (2013) anaeleza kuwa nyimbo za asili za Wahehe zimegawanyika katika makundi tofauti kama nyimbo za harusi, za matambiko, za jando, za kubembeleza watoto, za kuchapulisha kazi, za uwindaji, za kufurahia mavuno, za kuwaimbia watawala na nyimbo za kuomboleza msiba, pia ngoma zilitumika wakati nyimbo zilipoimbwa. Ngoma za Wahehe zinazojulikana ni livangala, miseya na kiduo. Nyimbo hizo huimbwa na kuchezwa katika kila wilaya kwa kiasi kikubwa na zina mfanano. Pamoja na yote hayo hakuna vitabu wala machapisho yanayoelezea juu ya nyimbo za asili za Wahehe kwa undani hususani nyimbo za asili za watoto.

1.3 Tatizo la Utafiti

Jamii nyingi za Kitanzania zimekuwa na utajiri wa nyimbo za asili zikiwemo za watoto. Thonya (1979) anaeleza kuwa wakazi wenye asili ya mkoa wa Iringa kama mikoa mingine wamekuwa na utamaduni wao, zikiwemo nyimbo za asili za watoto toka zamani. Kimsingi, nyimbo za asilia za watoto kama zilivyo nyimbo nyingine za asili na fasihi simulizi kwa ujumla zinakabiliwa na usasa unaotokana na kukua kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na mwingiliano wa kijamii kutokana na watu kuhamia sehemu husika kuathiri uhai wake (Kivenule, 2005).

Hapa Tanzania wapo wataalamu waliofanya utafiti wa nyimbo za makabila baadhi yao ni Miyuka (1990) ambaye amechambua wimbo wa jandoni, Mbangule (1961) amechambua wimbo wa siasa katika kabila la Wasukuma. Kutokana na msaada wa tafiti hizo mtafiti aliweza kubaini kuwa baadhi ya wataalamu wameelezea maana ya nyimbo na wakafanya utafiti katika makabila tajwa lakini hawajawahi kufanya utafiti kuhusu dhima katika nyimbo za asili za kabila la Wahehe.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza dhima katika nyimbo za asili za watoto katika kabila la Wahehe.

1.4.2 Malengo Mahususi

i) Kuchambua dhima za nyimbo za asili za watoto katika kabila la Wahehe mkoani Iringa.

ii) Kuelezea nafasi ya dhima za nyimbo za asili za watoto katika kabila la Wahehe.

1.5 Maswali ya Utafiti

i) Ni dhima zipi zinazojitokeza katika nyimbo za asili za watoto katika jamii ya Wahehe mkoani Iringa?

ii) Dhima za nyimbo za asili za watoto zina nafasi gani katika jamii ya Wahehe Mkoani Iringa?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unakusudia kuwanufaisha wanajamii kwa ujumla wake hasa juu ya

nyimbo za asili za watoto. Utafiti huu utakuwa umetoa nafasi ya kuzikumbuka nyimbo za watoto. Pia kuelewa dhamira za nyimbo hizo na jinsi dhamira hizo zinavyoweza kutumika kama nyenzo za kujenga maadili ya jamii yao.

Mulokozi (1996) anasema bado tunahitaji maandishi mengi zaidi yanayotokana na utafiti wa uwandani. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wanafunzi watayatumia matokeo ya utafiti huu kuwa ni sehemu ya madondoo yao ya kukamilisha madhumuni ya utafiti wao watakaokua wanafanya. Matokeo ya utafiti huu yatatumika kama sehemu ya kujikosoa au kujinoa ili kubainisha pengo la maarifa ambao wao watalijaza katika utafiti wao.

Utafiti huu utaweza kutumika na wataalamu ambao ni walimu, wahadhiri na maprofesa katika taaluma ya fasihi wataona umuhimu wa utafiti huu katika kuandika vitabu, makala na maandalio ya masomo ya kufundishia wanafunzi wao wa ngazi mbalimbali za elimu. Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika Taifa kwani utasaidia kufafanua nyimbo za watoto zisambae na kufahamika na wengi tofauti na Iringa. Watu watakaosoma utafaiti huu utawasaidia kubadilika kimtazamo na hivyo kuamsha ari ya udadisi zaidi na kuuelewa utamaduni wa watoto wa Iringa (wahehe). Kinadharia, utafiti huu umetoa uthibitisho kwamba nadharia ya uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaalamu kupitia utafiti huu, watafiti wa baadaye wataona umuhimu wa kutumia nadharia katika kutafiti kazi za fasihi.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu utajikita kutazama dhamira katika nyimbo za asili za watoto za Wahehe.

Mtafiti anakusudia kutazama zaidi ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizo na jinsi ujumbe huo unavyoweza kutumika kama nyenzo ya kuwaadilisha watu au kuwapotosha. Mtafiti hataingia kutazama vipengele vya fani. Kama mtindo wa nyimbo za asili za watoto. Kijiografia utafiti huu utafanyika katika wilaya ya Kilolo mkoa wa Iringa. Pia utafiti huu utajumuisha sampuli ya watu 48.

1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Kwa ujumla tasnifu hii ina sura tano zilizoelezea mambo mbalimbali ambayo yaliyosaidia kukamilika kwa utafiti huu wa nyimbo za asili za watoto za kabila la wahehe. Sura ya kwanza inahusu vipengele muhimu vya kiutangulizi vya utafiti ambavyo ni pamoja na usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu, malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa utafiti. Sura ya pili ya tasinifu hii imewasilisha mapitio ya machapisho na marejeo. Dhana ya nyimbo kwa ujumla, pengo la utafiti, nyimbo kama kipengele cha fasihi simulizi, nyimbo za asili kwa ujumla na nyimbo za watoto, dhima za nyimbo, dhima za asili kwa ujumla na nyimbo za asili za watoto, nafasi ya dhima mbalimbali za nyimbo za watoto za asili kwa jamii, kiunzi cha nadharia na pengo la utafiti. Sura ya tatu inahusu mbinu na njia za utafiti za kukusanya na kuchambua data. Sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti zinazohusiana na vipengele vya kifasihi juu ya nyimbo na kujadili data za utafiti na dhamira za kifasihi katika nyimbo. Pia katika sura ya tano ambayo ni ya mwisho iliyotoa hitimisho.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MACHAPISHO NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii ya mapitio ya machapisho yanahusiana na utafiti huu unaolengakuchunguza dhamira katika nyimbo za watoto za asili katika mkoa wa Iringa. Sura hii inahusisha vipengele vifuatavyo: Pengo la utafiti, dhana ya nyimbo kwa ujumla, (nyimbo kama kipengele cha fasihi na kazi zake), dhana iliyotumika katika nyimbo (nyimbo za asili na dhima), dhima za nyimbo kwa ujumla, nafasi ya dhima ya nyimbo za watoto, aina ya nyimbo za asili za watoto, dhima za asili kwa ujumla, nyimbo za watoto kwa ujumla na hitimisho.

2.2 Dhana ya Nyimbo kwa Ujumla

Nyimbo ni aina ya sanaa ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalumu. Mara nyingi nyimbo hutumia ala za muziki kama vile ngoma. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi. Wimbo hugawanyika katika beti na mishoshoro. Nyimbo nyingi huwa na kiitikio au mstari ambao hurudiwarudiwa.

2.2.1 Nyimbo Kama Kipengele cha Fasihi na Kazi Zake

Ili kuweza kuzijua nyimbo hususani nyimbo za watoto, utafiti huu utapitia na kusoma makala, machapisho na vitabu vilivyoandikwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi simulizi. Omary na Mvungi (1981) wanaeleza kuwa nyimbo zipo katika fasihi simulizi na ni za kimapokeo, kila kizazi kinapokezana nyimbo hizo, siyo kashfa, bali ni sifa mojawapo ambayo binadamu anayo. Kwa kuwa nyimbo hizi huathiri mtu

mmoja kwenda mtu mwingine, maneno fulani hubadilishwa kwa ajili ya kuandikwa au nyongeza ya msimuliaji katika masimulizi yake ili yapendeze. Mulokozi (1996) anafasihi nyimbo kuwa ni utanzu wa ushairi katika fasihi simulizi. Anaendelea kufafanua kuwa nyimbo ni kila kinachoimbwa na ambacho kinaambatana na muziki wa sauti, muziki wa ala, matini au maneno yanayoimbwa, kwenye sherehe, ibada na kilio. Mulokozi anaendelea kusema kuwa, nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa sana katika jamii za kiafrika. Hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto ili alale, kuchapulisha kazi na kutia hamasa vitani. Nketia (1963) anaeleza kwamba, nyimbo huelezea shughuli za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kidini. Nyimbo huimbwa kwa nyakati tofauti kuelezea matukio ya hisia tofauti kwa mfano huzuni, hasira, kulalamika, kuwasiliana na Miungu na kuomba uponyaji. Nyimbo nyingi za asili za makabila mengi ya Afrika huimbwa kufuatana na matukio maalumu.

Mwanza (2007) aliangalia mtindo katika nyimbo za watoto wa shule za Chekechea. Ameeleza kuwa, nyimbo za watoto wadogo ni budi ziandaliwe nyimbo fupi zenye maneno machache. Hii ni kutokana na uwezo wao wa kuyashika wanayofunzwa kwa urahisi. Naye msanii Thonya (1979) huyu anasema kuwa, ni muhimu sana kukumbuka na kuzingatia kwamba, watoto hasa wadogo hawana maelekeo ya kuzipenda nyimbo ambazo ni ndefu au zenye maneno mengi kwani wanashindwa kuzishika kiurahisi, hasa zile zenye ghani nyingi. Watoto wanapenda kuzishika kiurahizi nyimbo zenye maneno machache, zenye ghani chache na ziwe zinazorudiwa rudiwa. Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea zaidi kuwa mara nyingi

nyimbo za watoto huendana na michezo yao. Kuna wakati wasichana huimba na kucheza peke yao kutokana na aina ya michezo. Pia wavulana nao wana nyimbo zinazoambatana na michezo yao lakini pia zipo nyimbo wanazoshirikiana kuimba katika michezo. Mawazo haya yametusaidia kutambua kuwa kuna michezo ya watoto wa kiume na wa kike na tumeyatumia mawazo haya katika utafiti wetu.

2.2.2 Nyimbo za Asili kwa Ujumla na Nyimbo za Watoto

Baadhi ya wataalamu wameelezea asili ya nyimbo, mfano Mduma (2012), Chaligha (2008) kuwa chanzo cha wimbo kinahusishwa na historia ya mwanadamu. Mwanadamu alipoanza kutumia lugha, alianza na hisia, mtoto anapozaliwa hutoa sauti ambayo huashiria tafsiri fulani kama woga, njaa, maumivu. Nyimbo zilitumika kama njia ya mawasiliano katika masuala ya kijamii tangu utotoni hadi uzeeni. Katika kujaribu kuelezea asili ya nyimbo hasa nyimbo za watoto Wataalamu mbalimbali wanajaribu kueleza asili hiyo mfano Sengo (1985) anasema asili ya nyimbo za watoto ni hadithi za jadi zilizosimuliwa na kina bibi, babu na hadhira kwa nyakati za jioni kwenye vioto vya moto.

Kwa upande mwingine, Thonya (1979) anasema kuwa nyimbo za asili za watoto zimetokana na michezo ya watoto ambayo watoto wametumia zaidi mwelekeo wa kuiga matendo ya wazazi wao au watu wazima wengine katika jamii. Matendo wayaigayo huwa ni yale ya shughuli za watu wazima. Nyimbo hizo za watoto pia hunogesha michezo yao na watoto hufurahia wakishirikiana na wenzao. Hivyo basi, michezo na nyimbo hizo si kwamba wamefundishwa bali ni silika zao. Silika hizo zinawafanya waige kufuatana na maumbile yao (Thonya, 1979).

2.3 Aina za Nyimbo za Asili za Watoto

Nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii ya watoto. Nyimbo hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko watoto wakiwa wanacheza michezo yao, ambayo huonya, hufunza, hubembeleza watoto kutokana na silika wanazoigiza na kuimba, katika kuainisha aina za nyimbo, wataalamu wanaainisha nyimbo hizo katika makundi kama: nyimbo za kubembeleza watoto, nyimbo za kilimo, nyimbo za jandoni, Nyimbo za vitani, nyimbo za harusini na nyimbo za wawindaji. Mduma (2012), Chaligha (2008) wanasema nyimbo hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, huonya, hufunza, kuarifu, huomboleza, hubembeleza watoto na hata hutia hamasa.

Pia wakaendelea kusema nyimbo hutumika katika kuoga mwaka, kumsifu mtume, nyimbo za kilimo, uvuvi na nyimbo za vitani. Severe (2012) alichunguza aina za nyimbo za asili za watoto na watu wazima wa kabila la Wamatumbi na kubainisha kuwa zilifundisha na kuadibu. Utafiti wake umetusaidia kupanua uelewa wetu zaidi juu ya dhima za nyimbo za watoto za asili za jamii ya Wahehe.

2.4 Dhima za Nyimbo

Nyimbo zina dhima kubwa katika jamii kwani zimesheheni uhalisia katika jamii husika. Miongoni mwa dhamira hizo ni kama kutoa elimu, kuburudisha, kuadabisha. Mulokozi (1996) anasema nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa sana katika jamii za kiafrika kwani hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe na wakati wa mapumziko pia huonya, hufunza, hunogesha hadidhi, huomboleza na huarifu

2.4.1 Dhima za Nyimbo za Asili kwa Ujumla

Nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii (Mulokozi, 1989). Nyimbo hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati mwingine hutumika wakati wa mapumziko, pia nyimbo huonya, hufunza, huomboleza, hutumika katika kubembeleza watoto na hata kutia hamasa. Mulokozi (1996) Sengo (2009) na Balisidya (1987) wanasema nyimbo zina dhima kubwa sana katika kuendeleza jamii hudumisha na kuhifadhi mila na desturi. Wametoa mifano ya nyimbo za jando na unyago ambazo kwa asili kubwa hulenga kufunza na kuadibu vijana ambao hutayarishwa kuingia katika maisha ya utu uzima. Nao Muhando na Balisidya (1976) katika utafiti wao walioufanya kuhusu mila na desturi za jamii ya Wakaguru waishio Kilosa mkoa wa Morogoro na matokeo yake yaligunduliwa kuwa, nyimbo za ngoma zilitumika katika kurithisha mila na desturi za jamii hiyo ya Kikaguru. Pia nyimbo hizo ziliimbwa na akina mama walioolewa ambao waliwachukulia kama watu wazima na wenye uelewa.

2.4.2 Dhima katika Nyimbo za Asili za Watoto

Nyimbo za watoto ziliweza kusaidia kunogesha michezo yao na wakati mwingine ziliwaongoza kuwa na subira wakiwa wanasubiri kuandaliwa chakula (kupikiwa) ili wasogeze muda mbele. Thonya (1979) anasema nyimbo na michezo inawafundisha watoto kuwa waaminifu kwa wenzao, kuthamini, kutii sheria zilizokubaliwa na wengi, kwa njia ya kuimba na kucheza michezo hiyo ambapo wanajifunza misingi muhimu ya maisha ya jamii.

Nangwa na Mwajabu (2013) wanaelezea kuhusu nyimbo za watoto katika kabila la

Wazaramo wanasema kuwa, nyimbo za watoto ziliimbwa zaidi kwenye shughuli za jando, mtoto anapozaliwa na siku mtoto anapotolewa nje (siku ya arobaini) kama ishara ya kumkaribisha duniani. Jamii iliandaa chakula ambacho walishiriki wote huku ngoma zikipigwa na nyimbo kuimbwa ambazo ziliambatana na michezo.

Mbagule (1961) amechambua wimbo wa siasa wa kabila la Wasukuma, Sengo (2009) anasema nyimbo za Wamatumbi zilidumisha mila na desturi za Wamatumbi na zililenga katika dhamira ya kulea, kuhifadhi na kuendeleza mema ya mila na desturi hizo. Katika kuelezea dhamira kwa ujumla na dhamira katika nyimbo za asili za watoto wataalamu wengi wamegusa dhamira zinazofanana kwa mfano dhima ya kuelimisha, kuadabisha, kuburudisha, kuomboleza dhamira (Nangwa na Mwajabu, 2013; Sengo, 2009; Mulokozi, 1996; Balisidya, 1976; Thonya 1979 na Severe 2012).

2.5 Nafasi ya Dhima za Nyimbo za Asili za Watoto kwa Jamii

Wamitila (2006) anaelezea juu ya fasihi kuwa, kazi yoyote ya fasihi huwa na ujumbe na malengo mbalimbali ambayo hukusudiwa yaifikie jamii husika. Yale yote ambayo hukusudiwa yaifikie jamii huitwa maudhui. Hivyo basi Maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha dhamira, ujumbe, falsafa, msimamo na migogoro. Thonya (1979) anaendelea kueleza kuwa nyimbo za watoto zina manufaa yake kwani zinasaidia kuelimisha, kuburudisha, ukakamavu, kuwa mwaminifu katika jamii, kutii sheria, kupendana na waweza kudumisha mila na utamaduni wao. Nyimbo na michezo ya kufundishwa, Thonya (1979) anasisitiza lazima itilie maanani umri wa watoto, maumbile yao, mila na Jumuiya zao, vifaa vya kuchezea na nyimbo ziwe fupi fupi.

Pia Thonya (1979) aliweza kuzitenga nyimbo na michezo ya watoto katika sehemu kuu mbili zifuatazo kwanza michezo inayotumia maelekezo ya silika ya kuiga matendo ya wazazi wao au watu wazima wengine ambapo mara nyingi huwa ni shughuli za watu wazima mfano: kupika, watoto wa kike na kiume huiga kujenga, zikiambatana na nyimbo zao za asili. Dhamira zitakazoshughulikiwa katika utafiti huu ni pamoja na dhamira ya kuelimisha, kuadabisha, kuburudisha na kuchapulisha kazi.

Dhima ya kuelimisha katika nyimbo za asili za watoto ziliweza kuwafundisha maisha mbalimbali. Dhima hizo ziliwaandaa watoto kwa ajili ya maisha ya baadaye na yale maisha waliyoyaishi. Watoto walipata mafunzo mbalimbali yakiwaandaa kwenye utu uzima, lakini sasa hivi nyimbo hizo zinapotea kwani watoto wanaimba nyimbo za kisasa zaidi kutokana na usasa. Mulokozi (1996) alitaja dhamira hii ya kuelimisha na alikiri hayo.

Katika dhima ya kuadabisha hapo zamani zilichukua nafasi kubwa katika kuwaadabisha kwa maana ya kuwafanya watoto wawe na tabia njema, wawe na heshima katika jamii, nafasi hiyo sasa hivi inazidi kumomonyoka kutokana na **Utandawazi** uliojitokeza. Sengo, (2009) naye amelieleza hilo, kwa ufafanuzi kuwa nyimbo zilitumika pia kwa watoto (vijana) waliopelekwa jandoni ambapo nyimbo ziliimbwa ili kuleta msisitizo wa kuwaandaa vijana kuwa na tabia njema katika jamii. Nyimbo ziliwafunza watoto wa kiume kuwa wajasiri na wajibu wa kutunza na kusimamia familia. Wakati unyagoni watoto wa kike walifundwa kwa lengo la

kuwalekeza wajibu wao katika familia baada ya kufuzu wote waliimbiwa nyimbo mbalimbali

Sehemu kubwa ya nyimbo ilikuwa ni kuburudisha ingawa dhamira nyingine zilijitokeza kukidhi hayo yaliyotajwa. Watoto pia waliburudika na kunogesha michezo yao kwa nyimbo. Thonya (1979) alikiri hayo, kwa kueleza kuwa nyimbo za watoto huwasaidia kupata hamasa ya kucheza michezo yao, anaongeza kusema nyimbo na michezo ya watoto huendana pamoja. Watoto wanapenda kuimba nyimbo kwa sababu zinawafurarahisha.

Kwa ujumla dhima hii ya kuchapusha kazi hapo zamani watu waliimba nyimbo ambazo ziliwafanya wasichoke na hatimaye kujikuta wamemaliza kazi bila shida yoyote, uchovu pia hawakuuhisi. Hivyo, hata watoto nao waliimba kwenye shughuli za kulima, kupalilia, kutwanga mahindi na shughuli nyinginezo walizoshirikiana wakiwasaidia wazazi. Leo hii wakubwa na watoto pia hawaziimbi nyimbo hizo. Hivyo, tumeona kuwa ni jambo la busara kufanya utafiti huu ili kuziba pengo la maarifa.

2.6 Pengo la Utafiti

Kutokana na mapitio ya maandiko na machapisho mbalimbali ni wazi kuwa maandiko mengi yalijitika zaidi katika kuangalia dhamira, dhima na mitindo ya nyimbo katika baadhi ya makabila. Mwakasaka (1977) alifanya utafiti katika kabila la Wanyakyusa akabainisha dhima katika nyimbo za wanyakyusa. Kazi za watafiti hawa ziligusa dhamira za nyimbo kwa ujumla wake bila kuangalia kwa kina dhima

za nyimbo za watoto. Pili kazi za watafiti hawa ziliangalia nyimbo za makabila kama wamatumbi na wanyakyusa (kwa Mlokozi na Mwakasaka) hii inaonyesha kuwa nyimbo za asili za wahehe hazijafanyiwa utafiti bado. Hii inadhihirisha wazi upungufu, kama sio kukosekana kwa tafiti na maandiko juu ya dhamira za nyimbo na hasa nyimbo za asili za watoto.

2.7 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani (Mdee na wenzake, 2011). Kwa msingi huo nadharia hubeba mawazo, dhana au maelezo yatolewayo kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, chanzo, muundo, utendaji na mwingiliano wa ndani na nje. Pia, Sengo (2009) anafasili nadharia kuwa ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo mkuu wa mtu watu au jamii mahali fulani wakati fulani ni kwa sababu fulani, kwa mantiki hiyo nadharia ni dira ni mwongozo wa kukabili jambo kifalsafa, kidini, kimantiki, kijamii na kiutamaduni.

Williady (2013) anaeleza kuwa nadharia ni maelezo yakinifu kuhusu kitu, tajiriba, mafanikio au maangamizi yanayochomoza katika jamii. Hivyo, nadharia hufangamana na mambo mbalimbali ya jamii kama vile msimu, maarifa, tasinifu, mikabala na mienendo mbalimbali ya jamii.

Goran (1994) anasema nadharia ni falsafa au kikundi cha taarifa zilizoanzishwa kwa sababu ya msingi, zinazotetea ukweli fulani wa jambo linalokusudia kuelezea ukweli fulani au tukio fulani. Mfano mzuri nadharia ya maendeleo ya jamii ilikusudia

kuelezea utaratibu wa maendeleo ya jamii. Wafemenisti wa kijamii wamehitaji seti ya namna (mfumo) dira ya kufanya kazi utakaowawezesha na utakao mwelekeza kama dira yao katika kuelewa maendeleo.

Baada ya kupitia makala na vitabu mbalimbali na kuchunguza nadharia itakayofaa katika utafiti huu unaohusu dhamira katika nyimbo za asili za watoto katika kabila la wahehe, ilionekana kuwa nadharia ya Uamilifu, Uasilia na Uhalisia zinafaa zaidi kwa utafiti huu. Nadharia uamilifu inadai kuwa kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na lengo fulani, nyimbo zote za makabila ziliimbwa kwa malengo fulani na kuleta ujumbe katika jamii husika. Pia zipo nyimbo za asili ambazo wanajamii walirithi toka kwa mababu ambazo ziliendelea kuimbwa ingawa nyimbo nyingine zilitokana na matukio tofauti katika jamii. Matukio hayo mengi yalikuwa na uhalisi katika maisha uhalisia unatokana na neno asili yaani chimbuko au kiini cha mwanzo, uhalisia ni ule ukweli unaoweza kuthibitishwa katika jamii ambapo nyimbo ziliimbwa kutokana na ukweli wa maisha yaliyopo katika jamii. Mtafiti aliona kuwa nadharia hizo za uamilifu, uasilia na uhalisia zitaweza kumuongoza katika utafiti wake kwa kuwa, nyimbo zililenga kutoa malengo na ujumbe, zilikuwa chimbuko yaani kiini cha nyimbo kuimbwa na ziliakisi ukweli dhabiti katika maisha ya jamii.

2.7.1 Nadharia ya Uamilifu

Nadharia ya Uamilifu ni nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi ambayo kwa mujibu wa Wamitila (2006) waasisi wa nadharia hii ya uamilifu ni pamoja na Bronislaw Malinowski, Radcliffe Brown na Franz Boazi. Nadharia hii inatazama zaidi dhima na dhamira ya kazi mbalimbali husika. Vilevile, nadharia hii inadai kuwa kazi yoyote ya

fasihi lazima iwe na lengo fulani au ilenge kuleta ujumbe fulani katika jamii hiyo. Waasisi wa nadharia hii walitazama kila kazi ya fasihi au kipengele cha fasihi kina maana gani katika jamii husika. Kwa maana hiyo basi, nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika utafiti huu kuchunguza dhamira zilizopo katika nyimbo za watoto za asili za wahehe.

2.7.2 Nadharia ya Uasilia

Nadharia ya Uasilia, mtaalamu Ntarangwi (2004) anaeleza kuwa chanzo cha nadharia hii ya uasilia ni maisha hulka, mtazamo na mipangilio ya maisha kama yalivyokuwa katika ukweli wake wote. Kwa mtazamo wake Ntarangwi, ameona binadamu hurithi tabia zake binafsi na haja zake za kiasili na kujikuta anafuata bila hiari yake bali kusukumwa na nguvu za kijamii na kiuchumi na kundi alilozaliwa nalo. Hata hivyo umuhimu wa mambo hayo si sawa na kipindi fulani kinachotokea katika jamii kwa muda na kutoweka ghafla.

Mambo haya yanapaswa kuwepo na kuendelezwa katika hali ya kupokezana toka kizazi kimoja hadi kingine. Nguzo ya nadharia ya uasilia ni maisha kama yalivyokuwa yaani maisha asilia. Kwa hiyo lengo la kimsingi la utafiti ni kutoa picha ya maisha kama yalivyokuwa (kwa ukweli wake wote) ili kueleza misingi ya maisha yalivyo sasa. Wakati mwingine inasemekana kwamba uasilia hutoa picha halisi zaidi ya uhalisia hali kadhalika nadharia ya uasilia hutoa picha halisi ya uhalisia.

Nadharia ya uasilia huchagua maudhui maalumu ya kuzingatia. Mtaalamu wa bailojia Charles Darwin katikati ya karne ya kumi na tisa, alishikilia kwamba

binadamu alikuwa chini ya himaya ya maisha ya asilia na kamwe hakuwa na roho au uhusiano wowote wa kidini ulioko katika kaida za ulimwengu halisi (Ntarangwi, 2004). Nadharia hii imetusaidia kuchambua lengo mahususi la kwanza la utafiti wetu.

2.7.3 Nadharia ya Uhalisia

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004) anasema nadharia hii katika upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususani kwa lengo la kupinga mkondo wa ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo ya ukweli anazingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa uzoefu alionao mtu katika kutenda jambo. Vile vile wana uhalisia huamini demokrasia kama hali ya maisha na malighafi ya kuelezea maisha ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi na matokeo yanavyoweza kuthibitika.

Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi hupaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, na kweli. Hivyo basi hata picha za ulimwengu zitakazoimbwa na msanii, zapaswa kudhihirisha hali hiyo. Nadharia hii ina maana ya uwakilishwaji wa hisia wa mambo katika kazi za fasihi na ulipinga mkondo wa utanashati wenye maringo, dharau. Plato (427- 347 BC) Aristottle (384 – 322) wanaona kwamba mhalisia huamini katika matokeo ya mambo ya ukweli na anazingatia ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Kwa hiyo uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi hasa za kijamii zilizopo.

Nadharia imemsaidia mtafiti kujua uhalisia wa dhima katika nyimbo za watoto nyimbo za watoto za asili za Wahehe.

2.8 Hitimisho

Sura hii ya pili imepitia kazi tangulizi inayohusiana na mada ya utafiti ihusuyo nyimbo za asili za watoto za kabila la Wahehe, ili kubainisha pengo la utafiti.katika sura hii mtafiti amepitia kazi zilizoeleza nyimbo kwa ujumla, dhana za nyimbo, nyimbo za asili kwa ujumla na nyimbo za watoto. Dhamira ya nyimbo za asili na nafasi ya dhamira za nyimbo za asili.Mapitio ya kazi tangulizi yanaonesha hakuna utafiti wa kina uliofanywa katika kuchunguza dhamira za nyimbo za asili za watoto wa kabila la wahehe.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha mbinu na hatua zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data. Hivyo, sura hii imehusisha vipengele vya muundo wa utafiti, eneo la utafiti, aina ya data, njia za kukufanya data, ushuhudiaji, usahili, hojaji, sampuli na usampulishaji, mbinu za uchambuzi wa data na uzingatiaji wa maadili katika utafiti.

3.2 Muundo wa Utafiti

Ili kukidhi malengo ya utafiti huu mtafiti alitumia njia ya kimaelezo, Creswell (1998) anaelezea muundo wa utafiti kama ni mtazamo wa kifikra ambao unamwongoza mtafiti katika utafiti. Kothari (2004) akiuelezea mkabala wa kimaelezo anasema mkabala huu ni mkabala unaohusisha tathmini, mitazamo, maoni na tabia. Anaendelea kusema kuwa, mkabala huu unamwezesha mtafiti kufafanua maoni na maelezo yanayotolewa.

Njia ya kimaelezo ni mkabala unaozingatia upataji wa data katika uhalisia wake na tafrsiri inayotolewa na watafitiwa (Creswell, 1998 & Alvesson na Skoldeberg, 2009). Kupitia muundo huu, mtafiti alipata fursa ya kushiriki na alipata muda wa kuhojiana na watafitiwa ana kwa ana. Njia ya kimaelezo ni mbinu ambayo ilimpa nafasi mtafiti kufanya mahojiano ya kina zaidi ambayo huhitaji ujuzi na ukamilifu katika kumwongoza mhojiwa kutoa taarifa zinazohitajika.

3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huelezwa kuwa ni mahali ambapo utafiti husika ulipofanyikia kwa maana ya data za utafiti zilipokusanywa na pengine kuchambuliwa (Kothari, 2008). Katika utafiti huu eneo la utafiti lilikuwa ni Kilolo ambapo ni mojawapo ya wilaya za Mkoa wa Iringa. Katika wilaya ya Kilolo maeneo husika na utafiti huu ni pamoja na tarafa za Mazombe, Mahenge, Kilolo na Irole, maeneo hayo yakijumuisha lahaja za vadongwe, vasungwa, vanyategeta na vasagala. Maeneo yaliteuliwa kutokana na kuwapo kwa wanafunzi, pia kuna makazi ya watu ambapo shule za awali na chekechea zipo. Kwa hiyo maeneo haya yameteuliwa na mtafiti ili kukusanya data kwa kulinganisha mawazo yao na kujua maoni yao kuhusiana na dhima zinazopatikana katika nyimbo za asili za watoto katika kabila la wahehe.

3.4 Aina ya Utafiti

Utafiti huu umefanywa katika aina moja ya utafiti ambayo ni utafiti wa maskani. Maskani ni mahali ambapo wanaishi watu huku wakifanya shughuli za kuendesha maisha yao (Hesseler, 1992). Maskani aliyoyatembelea mtafiti ni yale ya Mazombe, Kilolo, Mahenge na Irole. Katika maeneo haya mtafiti alikusanya data za msingi kwa kutumia mbinu ya majadiliano rasmi na kundi la vijana, wazee na watoto.

3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa

Katika utafiti huu tumekusanya data za msingi na upili kama inavyowasilishwa hapa chini:

3.5.1 Data za Msingi

Neno msingi ni neno la Kiswahili ambalo hutumika kurejelea mwanzo wa jambo au

kitu muhimu sana kinachowezesha mambo mengine kufanikiwa. Katika utafiti data za msingi hutumika kurejelea data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza kabisa katika utafiti fulani na kwamba hazijawahi kukusanywa data hizo na mtu mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu anaofanya mtu huyo kwa wakati huu (Kothari, 2008). Data za msingi hukusanywa maskanini kwa mtafiti kufanya usaili, mahojiano au ushuhudiaji na ushiriki kuhusu mada yake ya utafiti.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu za ushuhudiaji, usaili na hojaji kama zilivyowasilishwa hapa chini:

3.6.1 Ushuhudiaji

Kushuhudia ni kuona tukio fulani wewe mwenyewe bila kuambiwa na mtu mwingine. Enon (1995) anaelezea kuwa ushuhudiaji unamfanya mtafiti aweze kushiriki katika tukio na kuona ukweli katika kupata data, mtafiti alishiriki darasani na kuona hali halisi ya wanafunzi wanavyoimba nyimbo za watoto katika shule za sekondari na shule za msingi wenye umri kuanzia miaka 7 wakiimba nje ya darasa ili kuona hali halisi wakiwa wanaimba kwenye michezo yao ya watoto. Mbinu hii imesaidia kuchunguza dhamira zilizotumika katika nyimbo kwa kuwa mtafiti aliweza kuona uhalisia wa uimbaji katika michezo ya watoto.

3.6.2 Usaili

Usaili ni mazungumzo yanayoambatana na maswali anayoulizwa mtu na mtu mwingine ili kudadisi taarifa fulani. Njia ya usaili hutumika kukusanya data, njia hii

hutumia mazungumzo kupitia maswali ya kuulizwa kwa mdomo au majadiliano. Mtafiti huwa ndiye mhojaji na mtafitiwa ndiye mtoa majibu. Njia hii ni ya mahojiano ya mwingiliano wa papo kwa papo (Walter, 1989).

Pia usaili ni njia mojawapo ambayo mtafiti aliitumia katika utafiti huu ili kupata data za moja kwa moja ambazo pia zilimwezesha mtafiti kupata data sahihi kutoka kwa wazee, wanafunzi na kisha baadaye kuyaweka katika maandishi. Majadiliano yalimwezesha mtafiti kukutana na wanafunzi ambao walikuwa na uwezo mzuri wa kujieleza na kujua dhamira za nyimbo zilizoimbwa na nafasi ya nyimbo katika kufunza maadili katika shule za sekondari na shule za msingi. Mbinu hii pia ilitumika mitaani kwa wazee ambao wamekuwa hawawezi kujieleza kwa njia ya maandishi, ama mtafiti alitumia mbinu hii kwa wazee ambao walimwimbia nyimbo ambazo alizinukuu na kisha kuzihakiki ili kupata data alizozitaka.

Kwa ujumla njia ya mahojiano hutumika kwa kuuliza maswali walengwa na kupata data kwa wale wasioweza kuandika na baadaye kuweka data hizo katika maandishi (Hessler, 1992). Mtafiti alitumia mahojiano ili aweze kupata ufafanuzi zaidi wa nyimbo alizokusanya na baadaye kuzihakiki kwa makini na kupata data sahihi kutoka kwa wanafunzi na wazee ili kupata mawazo na maelekezo yenye kufaa. Mahojiano haya yalifanikiwa kutokana na mtafiti kujenga mahusiano ya karibu yaliyopelekea kumwezesha kupata ufafanuzi wa kina katika nyimbo.

3.6.3 Hojaji

Hojaji ni karatasi yenye maswali ya uchunguzi. Maswali ya hojaji yalitumiwa na mtafiti kwa watafitiwa ambao waliweza kujibu maswali bila woga. Maswali

yaliandaliwa kwenye karatasi ambayo humfanya mhojiwa kuyajibu kwa kueleza kile alichoulizwa (Enon 1995). Kwa hiyo watafitiwa waliweza kujibu kulingana na ufahamu wao. Mtafiti alitumia njia hii ili kupata data za uhakika na kwa haraka na kwa kuwatumia wasaidizi maalumu wa utafiti huu wa nyimbo za asili za watoto za kabila la wahehe kwenye shule za sekondari, shule za msingi, shule za awali, shule za chekechea na watoto wa mitaani.Wasaidizi ambao walimsaidia kusimamia kujaza hojaji.Mtafiti alitumia njia hii ya mahojiano katika utafiti kwa kuandaa hojaji zilizo lenga kwa watafitiwa ambao walijibu kulingana na ufahamu wao.

Njia hii imetumika kukusanya data kwa wanafunzi wa sekondari 16, kutokana na sababu zifuatazo, kwanza inamfanya mtafiti wa aweze kujieleza kwa uhuru bila hofu kwa yale aliyoulizwa. Pia inamsaidia mtafiti kupeleka hojaji kwa watoa taarifa wengi na kujazwa kwa muda mfupi. Hojaji hizo zimewaruhusu watoa data kutoa maoni yao kuhusu jambo waliloulizwa, na pia zitawajengea hali ya kijiamini zaidi katika kujibu kile walichoulizwa na kukielewa.

3.7 Sampuli na Usampulishaji

Cresswell na wenzie (2009) wanaeleza kuwa sampuli ni idadi ndogo ya watafitiwa wanaoteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuwakilisha kundi hilo kubwa katika utafiti husika. Ni jambo lisilowezekana kwa mtafiti kulitafiti kundi kubwa kabisa la watafitiwa na kufanikisha kupatikana kwa data muafaka kwa muda mfupi na hivyo kulazimika kuteua watafitiwa wachache kutoka katika kundi hilo ambao wanawakilisha sifa za walengwa wote kwa ujumla wao. Hivyo basi sampuli ya utafiti huu ni ya wanafunzi wa sekondari walioteuliwa kwa kutumia usampulishaji

lengwa kwa sababu wana maarifa ya kutosha kuhusiana na mada ya utafiti wetu. Usampulishaji lengwa ni aina ya usampulishaji ambao humwezesha mtafiti kuteua sampuli ya utafiti wake akiwa na imani kwamba watafitiwa hao watampatia data anazozihitaji (Kothari, 2009).

Wanafunzi hawa waliteuliwa kwa sababu wao wamepitia michezo ya utoto ambayo waliicheza na kuimba. Pia, wanafunzi hao wanaweza kusoma na kuandika. Mtafiti aliteua vijana wanne kila tarafa. Jumla ya vijana watafitiwa ni 16. Watoto walikuwa 6 kutoka kila tarafa jumla ni 24 na wazee walikuwa 2 kila tarafa jumla ni 8. Hii ni sawa na kusema utafiti huu ulikuwa na wanamjadala 48. Idadi hii ya watafitiwa haikutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Jedwali lifuatalo limeainisha sampuli ya watafitiwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Utafiti Katika Jedwali

NO	KUNDI LA WATAFITIWA		TARAFA YA KILOLO			TARAFA YA MAZOMBE			TARAFA YA MAHENGE			TARAFA YA IROLE			**IDADI**
			JINSIA			JINSIA			JINSIA			JINSIA			
			ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	
1	WATOTO	7-13	3	3	6	3	3	6	3	3	6	3	3	6	**24**
2	VIJANA	20-30	2	2	4	2	2	4	2	2	4	2	2	4	**16**
3	WAZEE	60-70	1	1	2	1	1	2	1	1	2	1	1	2	**8**
	JUMLA														**48**

Chanzo: Mtafiti 2017

3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu yam kabala wa kimaelezo kama inavyoelezwa hapa chini:

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi usiokuwa wa kimahesabu ambao unajulikana kwa jina la mkabala wa kimaelezo (Babbie 1999). Kothari (2008) anasema kwamba, mkabala wa kimaelezo hutoa fulsa kwa mtafiti kuziainisha data zake katika makundi mbalimbali kulingana na mada ya utafiti na kisha kuzipanga kwa namna ambayo itakuwa rahisi kwake kufanya uchambuzi wa data zake. Baada ya hapo mtafiti huandaa mada kuu na mada ndogondogo ambazo zinaendana na makundi mbalimbali ya data alizounganisha. Hatua inayofuata ni kuzichukua data husika na kuzifanyia uchambuzi unaolenga kukamilisha madhumuni husika ya utafiti wake. Hivyo basi, katika kufanya uchambuzi wa data za utafiti, mtafiti aliziainisha data zote katika makundi mbalimbali yanayoendana na madhumuni ya utafiti huu na baada ya hapo tuliandaa mada kuu na ndogondogo kutoka katika madhumuni mahususi ya utafiti. Hatua ya mwisho ilkuwa ni kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti.

3.9 Maadili ya Utafiti

Uzingatiaji wa maadili ni moja ya hitaji katika utafiti (Kothari, 2008). Ili kuepuka madhara ya kutozingatia maadili katika tafiti, mtafiti alizingatia maadili ya utafiti kwa kuwa mwangalifu kutotoa siri, kutotaja jina na kutomlazimisha mtu kuingia kwenye utafiti, pia mtafiti alizingatia kutokosoa yale aliyoyakuta yakifanyika katika jamii husika.

3.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza vipengele mbalimbali na mbinu za utafiti. Vipengele hivyo

ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, aina ya utafiti, ushuhudiaji, usaili, hojaji. Pia, tumewasilisha vipengele vya watafitiwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii ya uchambuzi wa data imelenga kuwasilisha na kutoa ufafanuzi wa kina wa uchambuzi wa data zilizopatikana katika utafiti huu. Data za utafiti zimechambuliwa kwa kuzingatia malengo mahususi mawili ambayo yalikuwa ni kuchambua dhima za nyimbo za asili za watoto za Wahehe na kubainisha nafasi ya nyimbo za asili za watoto za Wahehe. Kutokana na ukaribu wa kimantiki wa malengo haya mahususi tumeyaunganisha katika uchambuzi wa data.

4.2 Dhima katika Nyimbo za Asili za Watoto za Wahehe

Lengo mahususi la kwanza katika utafiti huu lilikuwa kuchambua dhima za nyimbo za asili za watoto katika kabila la wahehe. Dhima zilizopatikana katika utafiti huu ambazo watafitiwa wamezitaja ni za kuhamasisha maadili mema, kuonya, kushapulisha kazi, kuenzi mila na desturi, kudumisha upendo, kuepuka uchawi, heshima kuagana na wazazi katika kuziangalia dhima hizo, mtafiti alitumia nadharia ya uamilifu, uasilia na uhalisia.

Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Watafitiwa Wanaokumbuka Nyimbo

KUNDI	**NDIYO**	**HAPANA**
Watoto	18	6
Vijana	12	4
Wazee	6	2
Idadi	36	12
Asilimia	**75%**	**25%**

Katika swali la kwanza la dodoso ambalo ni swali la mwongozo liliulizwa kwa watafitiwa kuwa je wanakumbuka nyimbo za asili walizoziimba wakiwa wadogo. Asilimia 75 walijibu ndiyo asilimia 25 walijibu kuwa wamesahau kama inavyowasilishwa katika jedwali namba 4.1.

Katika maswali yaliyoulizwa kwa watafitiwa, waliambiwa wataje nyimbo ambapo walizitaja nyimbo za harusi ambazo zilikuwa ni kuonya na kuelimisha mfano wa nyimbo hizo ni kama; nyimbo za kuelimisha, Twiyawe uwugona nzala, yangi mwaiwona, iligimilo ni nyengo, waisabula ikidulu cha munyidama. Nyimbo za kuonya; na lwa mtalo we undisile, kibudibudi kote uwukoko, nunza avana iva nene nunza, nene sungenyame nene ndapulike lukani. Dhima ya kuelimisha; ziliimbwa nyimbo zifuatazo haiyago, ve kabeva veve, vanangu mlikwiyaga, gondame winule iligobole. Dhima ya kuchapulisha kazi; kuna nyimbo zifuatazo, mbega mbega, kasuva vale, katuli katuli. Dhima ya mila na desturi; ziliimbwa nyimbo zifuatazo mganga ndagule, tonye ndonya tonye. Dhima ya kuagana na wazazi ziliimbwa nyimbo kama, kasuguni, gendelage wema, dhima ya heshima; ziliimbwa nyimbo kama, lingu lingu, uwifu mwiko mkomi gu mtela.imwene yailela vanu.

4.2.1 Kuhamasisha Maadili Mema

Thonya (1979), anaelezea kuwa nyimbo ziliwafundisha watoto misingi muhimu ya maisha ya kijamii. Maadili mema ni mojawapo ya dhamira ambazo watafitiwa wameitaja na kusema kuwa dhima hii hujitokeza katika nyimbo za jando na kuwafunda wari. Mtafiti alibaini kuwa wazazi waliweza kupata fursa kuonesha wajibu wao katika kuwaeleza watoto maadili mema wanayotakiwa kuyafuata na yale

watakayo kwenda kupambana nayo katika maisha yao kwa sababu watoto wa kiume na wa kike waliandaliwa kuwa wazazi bora wa familia zao.

Watafitiwa wanasema Wahehe waliwapeleka wavulana jandoni, wasichana walichaguliwa wenye umri unaolingana ambao wamevunja ungo, na wanaokaribia kuvunja ungo walipelekwa bondeni au kwenye miti mikubwa karibu na mto, huko walipatiwa mafunzo yahusuyo nyumba na unyumba. Mtafiti alibaini kuwa vijana wa kiume na kike walipofuzu mafunzo yao waliimbiwa nyimbo za kishujaa zenye mafunzo. Kwa hiyo watoto waliweza kuigiza na kuimba baadhi ya nyimbo walizoimbiwa vijana wakiwa wanatoka jandoni kama wimbo ufuatao:

Wimbo
Kiongozi: *Ligimilo ni nyendo*
Kibwagizo: *ye dado nu nyoko*
Kiongozi: *Ligimbilo ni nyengo*
Kibwagizo: *ye dado nu nyoko*
Wote: *kangalage ulimage, su la lya kumwaka x 2*

Tafsiri
Jembe na fyekeo (mundu)
Ni baba na mama yako
Ukakazane kulima, usije lala na njaa, mwakani.

Kuhamasisha maadili mema ni moja kati ya dhima za nyimbo za asili za wataoto katika jami ya Wahehe. Mazigwa (1991) anaeleza kuwa, nyimbo ni hazina ambayo husambaza mawazo juu ya maisha ya binadamu na maendeleo yake, kwa kufanya hivyo anasema nyimbo huweza kutoa mafunzo ya kuonya, kukosoa na kuadilisha jamii. Hivyo basi, watafitiwa wanasema wimbo huo uliimbwa jandoni pia hata harusini na watoto nao waliigiza haya kwenye michezo yao. Wimbo huo ulikuwa na nia na madhumuni ya kuwaasa na kuwaelimisha vijana kuwa wasikae na kubweteka

kuwa wavivu, vijana walielimishwa kutumia nguvu zao katika kilimo ili kuepuka njaa. Pia kwa wanandoa wimbo uliwahimiza wasiende kubweteka. Wimbo uliwahimiza wafanye kazi katika kilimo kwani hawatapatwa na njaa. Hivyo basi dhamira katika wimbo huu ilikuwa ni kuelimisha juu ya umuhimu wa kilimo kwa maana hiyo wimbo huu unaonesha ukubalifu katika nadharia ya uhalisia katika jamii. Ukiangalia katika maisha ya kila siku katika taifa, kilimo ni uti wa mgongo wimbo huu ni ujumbe tosha hata kwa makabila mengine.

Wimbo:
Waisabula kidulu cha mnyidama
Kiongozi: *Se kalongole ve mnyauhulo,*
pede si vakwigise ukwenu ava papo x 2
Pe wisabula ikidulu cha mnyakaye ndawuli x 2
Kiitikio : *Uyo mhonge mnyolage, aihongi nyoni x 2*
Lelage na vana valasapula
ikidulu cha mnyakaye iye
Kiongozi *Vana vavo*
Vasabula gu muhusi hela
Iyeba iyeba
Uyeba mama iyeba x 2

Tafsiri:
Wimbo huo unamsema kuwa Sekalongole ni mwanamke wa ajabu, je wakina bibi hawakukufunza unapochukua (kuopoa) kipaja cha kuku toka kwenye mchuzi, hujui ni mlo wa mwanamme. Uwafunze watoto wasitumie nyama, kwani watoto hutumia mchuzi.

Mulokozi (1996) anasema, nyimbo zinadhamira kubwa sana katika kuendeleza, kudumisha na kuhifadhi mila na desturi ametolea mfano nyimbo za jando na Unyago ambazo kwa asilimia kubwa hulenga kufunza na kuadibu vijana hivyo watafitiwa wanaeleza kuwa wimbo huo uliimbwa anapofundwa mwali, na pia anapoandaliwa kwenda kuolewa alionywa kuwa akiandaa nyama ya kuku huwa zipo sehemu maalumu ambazo anatengewa mume. Watoto hutumia mchuzi.

Hii ni moja ya heshima ambayo alipewa mwanamme wa kihehe. Dhamira inayopatikana hapa ni kuwa heshima ilitiliwa mkazo mke kumheshimu mume na watoto kuheshimu wakubwa kwa kuhusisha nadharia ya uasilia wimbo huu unakubaliana na nadharia hiyo kwani toka zamani wakubwa waliheshimiwa na wadogo, wanawake waliwaheshimu wanaume na kila mmoja alitimiza wajibu wake. Hata kwa makabila mengine ya Tanzania wengi walifanya hivyo ingawa mila za kuachiwa wanaume wale vitu vizuri imepitwa na wakati haifai kuigwa.

4.2.2 Kuonya Jamii

Watafitiwa waliitaja dhima ya kuonya jamii kuwa imejitokeza katika nyimbo za kabila la Wahehe. Dhima hii ilitajwa na watu wazima. Watafitiwa waliimba nyimbo ambapo waliweza kutaja dhamira na mtafiti aliweza kubaini na kuzichambua ili kuziweka katika makundi ya dhamira zinazoelekeana.

Dhamira ya kutoa maonyo hujitokeza katika nyimbo zifuatazo

Wimbo
Na lwamtalo we undisile kangi
Uwilye amatata gako x 2

Kibwagizo
Kumahame be x 2
Be be be be amatata gako
Kumahame be kumahame be x 2

Tafsiri
Hapo nyuma ulishanitukana tena leo hii umerudia uchokozi wako kwenye makazi ya zamani
We we we we makazi ya zamani

Mulokozi (1996) ameeleza kuwa nyimbo za maadili ya kuonya ziliiimbwa na makabila yote ya Kiafrika ambazo zilikusudia kuwaasa watoto na vijana. Hivyo wimbo huu unaonesha Uhalisia uliopo, kwa hiyo katika wimbo huo Mahame ni mahali walipoishi watu zamani na baadaye wakahamia sehemu nyingine wimbo huu uliimbwa na kuchezwa na watoto wakiigiza kuhamia vijiji vipya. Watoto waliigiza ugomvi na kuonyana kwa kuimba wimbo kama huo. Wimbo huu ulimwonya mtu kutokana na tabia ya kurudiarudia kutukana wenziwe, mtukanaji alionywa kutorudia tabia hiyo inayowakera wengine. Nadharia ya uamilifu inafaa kwani inaeleza kuwa kazi yeyote ya fasihi huwa ni kupata ujumbe fulani. Wimbo huu unalenga kutoa ujumbe kwa mhusika wa uhalifu. Katika jamii wako watu wa namna hiyo ambao hujifanya wababe kutoa lugha zisizofaa kwa wenzao hivyo wanapaswa wabadilike ili wakubalike na kuishi kwa amani na wenzao lugha za matusi hazifai ili vizazi vyetu viige yaliyo mema

Wimbo

Kiongozi :	Nunza vana iva nene nunza x 2
	Si va ndema
Wote :	Nunza vana iva nene nunza x 2
	Si va ndema
Kibwagizo :	kumbatilake vana vakiva kumbatilage x 2
	Se yuva: kumbatilage vana vakivakumbatilage

Tafsiri

Nitatunza watoto hawa mimi nitatunza x 2
Nitatunza hawatunishinda
Wakumbatie watoto hawa wakumbatie ni wakiwa (yatima)

Ntarangwi (2004) anamtaja Charles Darwin aliyezuka karne ya 19 ambaye anadai kuwa ukweli unaozingatia na kupewa kipaumbele ni ule unaoweza kuonekana wazi.Watoto waliimba kwa kuigiza uyatima kwa kuimba wimbo kama huo

ulivyoonyweshwa hapo juu. Hivyo basi wimbo huu huimbwa ili kumuonya mtu ambaye amepewa au amewachukua watoto yatima ili awatunze. Anaambiwa awatunze awe jirani nao. Naye mhusika huitikia kuwa atawalea hawatamshinda kwa maana hiyo mtunzaji anakuwa amepokea onyo alilopewa. Nadharia ya uhalisia inaendana na wimbo huu kama tunavyoelewa katika jamii watu walio wengi huwa hawawatunzi watoto yatima kwa upendo wa dhati. Watoto wengi wanaopitia hali hii hunyanyasika na wale wanaowalea kwa kuwa si watoto wa uzao wao.

Pia katika makabila mengine wapo watu ambao si msaada kwa watoto yatima hata kwa watu wasiojiweza. Tunatakiwa tuwajali wenzetu wasio na msaada pale inapobidi watoto yatima ni wengi kwenye jamii zetu. Wasitengwe tuwajali kwa kila hali.

4.2.3 Kuelimisha Jamii

Kuelimisha jamii ni dhima ya nyimbo za asili za watoto za kabila la Wahehe ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa. Mulokozi (1996) anasema kuwa, nyimbo zina kazi kubwa sana katika kuiendeleza jamii, kudumisha na kuhifadhi mila na desturi ametolea mfano nyimbo za jando na unyago ambazo kwa asilimia kubwa hufunza, huadibu vijana ambao huandaliwa kuingia kwenye utu uzima.

Wimbo wa haiyago namna unavyoimbwa, huimbwa wakati watoto wakiwa wamejipanga mstari mmoja. Idadi ya watoto wanaweza kuanzia sita hadi kumi na tano. Mbele ya hao watoto anakuwepo kiongozi ambaye huwa ni mjanja na jasiri. Watoto wanajipanga mstari mmoja kurudi nyuma huku kiongozi wao akiwa

ametangulia na kila mmoja hushika nguo zilizofungwa kiunoni kwa nguvu nyuma ya mtoto aliyetangulia. Nguo hizo kiunoni hufungwa fundo kwa nyuma. Mbele ya kiongozi huwepo mtoto aliyesimama akitazamana na kiongozi umbali wa hatua moja hadi moja na nusu. Huyo huwa ni adui. Nia ya adui huyo ni kufanya kila njia kuwapata wale walio nyuma ya kiongozi wao, iwe kwa kuwagusa au kuwashika anakuwa amewateka. Mateka hao kuhamia kwa adui. Kiongozi anatakiwa kufanya kila njia ya kuwakinga watu wake wasitekwe. Huwakinga kwa kunyoosha kando mikono yote miwili. Wanapoendelea na mchezo huo wimbo huimbwa. Lakini endapo adui atashindwa. Kiongozi na watu wake watajikusanya na kuunda duara na kuimba wimbo wa ushindi

Wimbo:

Adui :	*Haiyago, haiyago*
Wote :	*Haiyago, haiyago*
Kiongozi,	*ndembwe ya kumilanzi mwaivasile eee*
	Ndembwe ya kumilanzi mwaivasile
	Lupembe lwelu x 2 (wote wanarudia)
Kiongozi :	*Vayawe vatofile yigwe yina huteee*
	Vayawe vatofile yigwe yina hute saba, tatu x 2 (wote wanarudia)

Tafsiri

Nyie nyie, nyie nyie
Tembo, huko porini alikufa akiponzwa na pembe yake nyeupe
tembo aliipigwa kwa bunduki yenye risasi saba mpaka tatu.

Ntarangwi (2004) anamtaja Charls Darwin kuwa ukweli hupewa kipaumbele na anapembua ukweli uliopo katika maisha.Watafitiwa wanasema kuwa watu walijitoa mhanga kutetea jamii zao na wimbo huu uliwafundisha watoto wawe shujaa. Pia ulimfunza kiongozi awe shujaa atetee watu wake kwa hali na mali. Nadharia ya uhalisia inaendana na wimbo huo kwani katika jamii kulikuwa na walinzi wa jadi ambao walipigana kufa na kupona ili kutetea jamii yao. Pia walipokuwa wakipigana

na makabila nje ya jamii yao na kushindwa walisherehekea kwa kuimba nyimbo, hata makabila mengine ya Tanzania walikuwa na utaratibu wa walinzi wa jadi kuilinda jamii. Na waliimba nyimbo za ushindi.

Wimbo
Paka na panya
Kiongozi : *ve kabeva veve kabeva veve*
Wime bado

Wote *:* *si ngwimwa x 2*
Kibwagizo *:* *Wime baho*
Singwima
Nige wime baho
Singwima

Tafsiri : *Kapanya wewe x 2*
Simama hapo hapo
Sisimami
Simama hapo
Sisimami
Simama
Sisimami

Watafiti wanasema wimbo uliimbwa na watoto wakiwa wamesimama katika duara na kushikana mikono yao kwa nguvu. Wakati huo huo mtoto mmoja alikaa katikati ya duara na kusimama badala ya panya, na nje ya duara huwepo mtoto mmoja anayesimama badala ya paka. Kazi ya paka ni kuhakikisha anapangua mikono kwa kuachanisha ili amfikie panya akifanikiwa kupenya humfukuza panya na kumkamata. Waliosimama nje ya duara kuhakikisha panya hatoki kwa kumzuia arudi ndani ya duara. Paka akishinda huchaguliwa wengine na wimbo huimbwa upya. Mchezo huisha pale watoto wanapochoka.Ntarangwi (2004) akimtaja Charles Darwin ambaye alizungumzia ukweli juu ya maisha ya ulinzi wa jamii. Wimbo huo huelimisha watoto waweze kubuni mbinu ya kumkwepa adui pia watoto wanakuwa wakakamavu. Nadharia ya uasili inaendana na wimbo huu kwa maana kwamba tokea

enzi za mababu watoto walifunzwa mbinu za kujihami na maadui. Sengo (2009) anazungumzia juu ya fasihi kuwa ina kwao kila jamii iliweza kubuni mbinu za maisha hata katika kujihami. Jamii wasikubali kushindwa, katika mapambano na watoto wanapaswa kufundishwa mbinu za kupambana na maaduni na kujiweka imara na kuufanya mwili uwe kakamavu

Wimbo :

Mama : *Vanangu muli kwiya*
Watoto *:* *Tulibaha*
Mama *:* *Muyiwene nyalupala*
Watoto*:* *eeh*
Mama *:* *ya kuilivata nyalupala*
Watoto*:* *eeh*
Mama *:* *Kangi ng'ali hilo*
Watoto *:* *Eeh*
Mama *:* *Yawulige dada*
Yawulige yuva
Neke yiwulage kuku
Mkoli ngolo
Watoto*:* *Uwii uwii uwii*
Mama *:* *mwangufye muhege*

Tafsiri

Mama *:* *Wanangu mko wapi*
Watoto*:* *Tupo hapa jirani*
Mama *:* *Mmemwona simba*
Watoto *:* *Ndiyo*
Mama *:* *Mwenzenu sina nguvu ya kupambana na simba tena simba ni mkali*
Aliua baba
Akaua mama
Tena akamwua babu
Pigeni kelele
Watoto*:* *uwi uwi uwi*
Mama *:* *fanyeni haraka mkimbie*

Ntarangwi (2004) kwa upande wake anaeleza juu ya hulka, mtazamo na mpangilio wa maisha kuwa binadamu amerithi tabia zake na haja zake za kiasili.Pia watoto wamerithi yale wanayoyaona kwa wazazi wao. Watafitiwa wanaeleza kuwa, wimbo huu uliimbwa kwenye eneo pana kama kiwanja cha michezo. Panakuwa na watoto

waliojipanga katika mstari kimapana kufuata uwanja wa kuchezea katikati ya uwanja huwekwa mtoto mmoja ambaye ni simba (adui) akitazamana na watoto walojipanga. Mwishoni mwa uwanja nyuma ya simba anakuweka mtoto mmoja anayeigiza kama mama. Mama huanzisha wimbo huo watoto nao huitikia anapotoa amri ya sasa kimbieni. Simba hujitahidi kukamata watoto ambao hukimbia kumfuata mama yao. Kila anayekamatwa anajiunga na mtoto aliye simba ili kumwongezea nguvu ya kuwakamata wengine. Akiwagusa au kuwakamata huwa mateka. Hivyo basi mchezo unapoanza tena simba wanakuwa wameongezeka. Mchezo huendelea mpaka adui wanapokwisha wote.

Guma (1967), anaeleza kuwa nyimbo ni chombo kinachotoa mwongozo wa tabia za watu kwa mtu mmoja au jamii kwa ujumla ambapo nyimbo huibua mawazo yanayoisaidia jamii kuyapokea na kuyafanyia kazi kama mwongozo wa maisha. Watafitiwa wanaeleza kuwa wimbo huu unalenga kuwafundisha watoto kuwa shujaa, kutumia mbinu kumkwepa adui kwani watoto katika mchezo huu hufurahi wanapofanikiwa kumshinda adui. Pia inakuza uwezo wa kukimbia kuufanya mwili uwe mkakamavu. Pia wimbo huu uliwafanya watoto watii amri wanapoamrishwa na wakubwa. Nadharia inayolandana na wimbo huu ni nadharia ya uasili. Watu wa zamani walikuwa na asili ya kutii amri wanapopewa. Pia katika jamii ya Tanzania watu walitumia nyimbo hizi kuwafunza watu watii sheria, amri za viongozi wao.

Wimbo
Gondame x 3
Winule ligobole x 2

Tafsiri
Inama x 3
Chukua pesa x 3

Wimbo huu unachezwa na watoto wawili katikati ya duara. Wengine wakiwa wanapiga makofi wakiwa wamewazunguka. Watoto hao hutazamana wakiwa wamejishika kiunoni kwa mikono mwili. Katikati yao huwekwa pesa iwe ya noti au sarafu. Wimbo unapoendelea kuimbwa watoto hao wawili hunesanesa wakielekea chini hadi kupiga magoti baadaye huinama na kuichukua pesa kwa kutumia mdomo huku mikono ikiwa kiunoni atakayewahi kuiokota kwa mdomo ndiye mshindi. Wimbo hurudiwa rudiwa kwa kupiga makofi na watoto wengine wakiwa kwenye duara. Wimbo huu unahusishwa na nadharia ya uhalisia kwa ukweli uliopo watafitiwa wanasema ili mtu apate pesa lazima ainame kwa kufanya kazi. Pesa haiji hivi hivi. Kwa jamii mafunzo haya yapo mtu anatakiwa afanye kazi ili amudu maisha. Hivyo wimbo huu ulikuwa unawaelimisha watoto jinsi ya kuishi.

4.2.4 Kuchapulisha Kazi

Kuchapulisha kazi ni miongoni mwa dhima ya nyimbo za asili za watoto wa jamii ya Wahehe ambazo watafitiwa katika wilaya ya Kilolo waliitaja. Kimsingi, katika jamii za Kiafrika zilizo nyingi zilitumia nyimbo wakati wa kufanya kazi hasa wakati kazi hizo zilipowahusisha watu wengi au kufanya kazi kwa kushirikiana, wakati mwingine watafitiwa wanasema kuwa hata mtu mmoja aliweza kuimba akiwa anafanya kazi nyimbo ilimpa moyo wa kufanya kazi na ilimwondolea uvivu na uchovu. Pia, Wahehe ni miongoni mwa makabila linaloimba nyimbo za kazi kama kilimo. Kutwanga na shughuli zingezo, hivyo basi watafitiwa wanasema nyimbo za asili za watoto wa kabila la wahehe zililenga kuwafundisha watoto jinsi ya kurahisisha utendaji wa kazi kwa kuimba nyimbo. Miongoni mwa nyimbo za kuchapulisha kama zilivyotajwa na watafitiwa ni hizi zifuatazo;

Wimbo
Kingozi : Mbega mbega
Kibwagizo : aye mbega x 2
mbega si munu
aye mbega
mbega likoko
aye mbega
mbega si miho
aye mbega

Tafsiri
mbega ni jina la mnyama nyati. Tafsiri ya wimbo
nyati nyati
haya nyatu
nyati si mtu
aya nyati
nyati si macho
aya nyati
nyati ni dudu la kuogopwa

Wimbo huu huimbwa wakati wa kufanya kazi kwa kushirikiana. Kama kwenye kilimo wahehe hualikana na kulima kwa pamoja kwenye shamba la mmoja. Kualikana huku wahehe waliita (mgove). Watoto nao katika michezo yao huigiza kulima na kuimba nyimbo za kuchapulisha kazi kama wimbo huo hapo.Ntarangwi (2004) awazungumzia kuwa maisha ni mpangilio ambao upo katika haja zake za kiasili kwa kusukumwa na nguvu za kijamii. Watafitiwa wanasema wimbo huo ulitumika kwenye shughuli kama za kupiga mahindi na watoto hupenda sana kuimba nyimbo hizo na hapo ndipo kazi kama hizo hufanywa kwa umoja na watoto au vijana wakiwa wanalima kwa umoja wao, wote humyanyua majembe juu kwa pamoja na kutua chini (kulima) kwa pamoja kama kupiga mahindi wote hunyanyua miti ya kupigia juu kwa pamoja na kutua kwenye mahindi kwa pamoja wakitumia nguvu na wimbo ukiwa unaendelea kuimbwa. Nadharia ya uasilia inaweza kufaa kwani tokea enzi za mababu zetu kazi hizi za kualikana zilikuwepo na watu walishirikiana katika

shughuli za kijamii. Hapo zamani makabila mengi yalikuwa yakifanya kazi kwa ushirikiano, hivyo katika jamii watoto watajifunza kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Nyimbo za kuchapusha kazi huimbwa katika hali ya kuigiza hatimaye watoto hujikuta wamekamilisha kazi waliyokuwa wanaifanya bila kuchoka.

Wimbo
Kasuva vale
Kasuva vala valage tugende
Tugende kwa si ulaya kutali
Kutali kulikadege kalonzi
Kalonzi kafalingundi mgendela
Ee kungulinguli msigala

Tafsiri
Kajua waka wakaga tusafiri
Tusafiri kwenda ulaya mbali
Mbali kunakandege kasemaji
Kasemaji kanajikita kwenye vumbi
Mkakatembelee

Ntarangwi (2004) anasisitiza kuwa binadamu huishi maisha ya kupangilia shughuli zake ambazo amezirithi toka kwa jamii anayoishi nayo. Watafitiwa wanaseama nyimbo hii iliimbwa asubuhi wakati watoto wakiamka mapema kwenda kwenye shughuli ya kutwanga nafaka kama Mahindi, kutwanga kunde na nafaka zingine kwa kutumia kinu. Ambapo kazi ya kutwanga ilifanyika na watu wawili, au mmoja hadi watatu wakishirikiana kutwangia kinu kimoja. Wimbo huu unaonesha ukubalifu na nadharia ya uhalisia na uamilifu. Uhalisia unaoangalia zaidi kazi pamoja na kuchapusha kazi. Pia katika jamii tunajifunza kuwa kazi inapofanywa na wengi huwa ni nyepesi, makabila mengi hapa nchini walifanya kazi kwa kushirikiana huku wakiimba nyimbo ambazo ziliwapa moyo wa kufanya kazi.

Wimbo

Kiongozi: *katuli katuli* x 2
Kiitikio : *katuli*
Kiongozi : *Nwanze nwanze* x 2
Kiitikio: *katuli*
Kiongozi : *Twitwangila nani*
Kiitikio : *katuli*
Kiongozi : *Katuli kaga ludama*
Kiitikio : *katuli*
Kiongozi: *katuli bela katuli*
Kiitikio : *katuli*
Kiongozi : *kangale* x 4
Kiitikio: *katuli*

Tafsiri

Kiongozi : *kinu, kinu*
Kiitikio : *kinu*
Kiongozi: *nisaidie kutwanga*
Kiitikio: *kinu*
Kiongozi: *tunamtwanga nani*
Kiitikio: *kinu*
Kiongozi: *kinu hakina ubishi*
Kiitikio: *kinu*
Kiongozi: *kinu hicho kinu*
Kiitikio: *kinu*
Kiongozi: *kazana*
Kiitikio: *kinu*

Watafitiwa wanasema wimbo huu hupendwa sana na watoto, huutumia katika kazi. Wimbo huu huimbwa wakati wa kutwanga pia hata kazi nyingine wanazosaidiana watu kwa umoja wao, kama vile kusogeza tofari katika ujenzi, wanapokoroga pombe za matambikio ili mradi ni kazi zinazofanywa kwa kushirikiana ikishirikisha watu zaidi ya mmoja. Wimbo huu huwa unamfanya mtu asichoke. Wimbo huu tunaweza kuuhusisha na nadharia ya uasilia kuwa tokea enzi za mababu zetu watu walialikana katika kusaidiana kazi. Ili kazi ifanyike kwa mara moja. Na katika makabila mengine kitendo hiki cha kusaidiana kipo na bado baadhi ya maeneo wanadumisha mtindo huu wa kualikana.

4.2.5 Kutunza Mila na Desturi

Katika kuielezea dhima hii watafitiwa wanasema mila na desturi za makabila hususani kabla la Wahehe zinazidi kuporomoka hivyo ni muda mwafaka tuanze kurudisha taratibu mila zinazotufaa. Zikiwemo nyimbo za makabila kudumisha tamaduni zetu. Katika mafunzo haya ya mila na desturi watu waliliwazana wakati wa msiba, sherehe na uvunaji wa mazao, kiongozi anapopita au kuwatembelea, kutibu ugonjwa, jando na unyago na matambiko. Kwa mfano nyimbo zifuatazo:

Wimbo

Kiongozi : *Mganga ndagule x 3*
apamwinga, mganga ndagule apamwinga ndina litego
Kumutwe konoo kwivava ndawuli x 2
Mganga ndagule apamwinga mganga ndagule apamwinga ndina litego
Mwileme umu mukave ndaule x 2 mganga ndagule apamwinga, mganga ndagule apamwinga ndina litego

Tafsiri: *Mganga niague x 2 niague (tabiri)*
Pengine ninaweza kuwa nimelogwa
- *Tumbo hili linaumaje mganga niague nisije kuwa nimelogwa*
- *Kichwa hiki kinaumaje mganga niague pengine nimelogwa*

Watafitiwa wanasema huo wimbo huimbwa na watoto wakiigiza yale wanayoyaona yakifanyika. Wimbo huu huimbwa kwenye matambiko pia kwenye misiba. Seif (2011) yeye anaonesha kuwa awali jamii iliweza kurithisha mila na desturi ya kizazi kimoja hadi kingine kwa kutumia nyimbo, watoto walilithishwa shughuli za mila kama matambiko. Hivyo nyimbo hii kuimbwa kuonyesha aliyekufa hakufa kifo cha kawaida wanafamilia wanapaswa kwenda kwa mganga wa jadi kujua siri ya kifo kile. Mara nyingine huimba katika matambiko ili kuomba misaada kwa miungu

yaani mizimu ili iweke wepesi wa mambo. Nadharia ya uhalisia inaendana na wimbo huu kuonyesha kuwa mila na destori zilidumishwa hata kwenye makabila mengine hapa nchini walifanya matambiko, kulikuwa na waganga wa jadi. Ingawa mambo hayo sasa yameanza kupotea.

Wimbo
Tonye ndonya tonye
Tonye mholo honde tonye
Vadada, vayuva, vakuku, va papa
Twisuka indonya yiyonye
Yitonye, yitonye, twisuka yitonye
Hegele ve gufufu veve
Tonye mholohondo tonye

Tafsiri
Nyesha mvua nyesha
Nyesha kwa wingi nyesha
Baba, mama akina babu bibi
Sogea wewe wingu zito
Mvua inyeshe nyingi

Seif (2011) na Mulokozi (1996) wanazungumzia juu ya kudumisha kuendeleza na kuhifadhi mila na desturi, zamani watu walifanya matambiko mvua zilipoacha kunyesha katika hali ya kawaida. Watafitiwa wanaeleza kuwa watoto waliimba wakiigiza kuomba mvua inyeshe hasa walioona wingu zito angani. Dhima tunayoipata hapa ni jinsi watoto walivyoona wazee wakitambika na mvua zilinyesha, kwamba mila na desturi zilikuwa na umuhimu katika tamaduni za makabila mbalimbali kwani waliona manufaa ya mvua. Wimbo huu pia unakubaliana na nadharia ya uamilifu na nadharia ya uhalisia, kuwa, kila kazi ya fasihi huwa na ujumbe uliokusudiwa na katika makabila mengi walifanya matambiko kwa ajili ya kuomba mvua wakati wa ukame hasa mvua zilipochelewa kunyesha.

4.2.6 Kupiga Vita Uchawi

Kupinga uchawi ni miongoni mwa dhima za nyimbo za asili za watoto za jamii ya Wahehe ambazo zimetajwa na watafitiwa ya kuwa watu walishikana uchawi mahali walipomhisi mwanajamii kuwa ni mchawi. Hivyo, mchawi aliogopa kuendelea kuwatesa wenzake ambapo wanajamii waliimba nyimbo kumtarifu juu ya uchawi wake.

Wimbo
Nene sunge nyame nene
Ndapulike lukani x 2

Kibwagizo
Amahavi iga
Gagaya wema

Tafsiri:
Mimi mpaka nihame
Nilisikia maneno
Wachawi hawa
Hawana wema
Hawana wema x 2

Watafitiwa wanasema watoto waliweza kuigiza, uganga, uchawi na waliimba baadhi ya nyimbo za kiuchawi. Sengo (2009) anaeleza kuwa kazi ya fasihi laziwe iwe na wajibu, wimbo huu uliimbwa ili kutoa ujumbe kwa watu waliokuwa wanaishi kwa kuamini uchawi. Wachawi walikuwa naogopwa pia walikuwa wanakera hivyo nadharia inayoendana na wimbo huo ni nadharia ya uamilifu. Kwa kuwa wimbo huo huimbwa kumsema mchawi kama yupo kwenye kundi hutoa ujumbe ili mhusika ajitambue. Katika jamii za kiafrika mambo haya ya uchawi yapo na yanarudisha nyuma maendeleo ni vyema watu wabadilike waachane nayo.

4.2.7 Kuagana na Wazazi

Watafitiwa wanadai kuwa katika kabila la Wahehe kulikuwa na nyimbo ambazo ziliimbwa kwa ajili ya kumuaga binti, kabla ya ndoa na binti alipewa mawaidha ya maisha ndipo binti aruhusiwe kwenda kuishi na bwana. Watafitiwa waliyaeleza hayo kupitia nyimbo zifuatazo ambapo mtafiti alielekezwa kuwa ni nyimbo za kuagana na wazazi. Hata watoto waliimba kwa kuigiza toka kwa wakubwa zao.

Wimbo wa kusuguni
Kiongozi : *kasuguni*
Kiitikio *:* *mlelembwe*
Kiongizi*:* *yuva ndindulile*
Kiitikio *:* *hamba ngalave*
Umwanangu hamba

Tafsiri: *Kasuguni ni nifungulie. Wanasema mama nifungulie, ili nikamwone mwanangu haya nikamuone mwanangu haya.*

Ntarangwi (2004) anamtaja Charles ambaye alizuka karne ya 19 akizungumzia ukweli na uhalisia uliopo katika maisha ya binadamu kwani binadamu walifanya shughuli zao halisi zilizoko kwenye jamii zao.

Wimbo huu huimbwa wakati wa harusi wanapomuaga mwali ili akaanze maisha ya ndoa. Watoto hujipanga mistari miwili mbele yake bibi harusi anakaa kwa kufunikwa nguo usoni. Wakati huo huo watoto huimba kwa kuruka juu na kupigiza mikono yao mwili. Kiongozi anaposema yuva ndindulile wanachezesha miguu na kurudi nyuma. Kiongozi akisema kasuguni wanasonga mbele. Nadharia ya uhalisia inaendana na wimbo huu kwani hueleza hali halisi ya maisha ya binadamu tabia hii ya kuaga binti anapoolewa ni ya kurithi toka vizazi na ni msukumo wenye nguvu katika jamii, ambapo makabila mengi katika Tanzania hufanya hivyo. Kumuaga binti

na kumpa wosia ili akienda kwenye jamii nyingine akaishi kwa kufuata maadili mema. Mila hii bado inadumishwa watu wa sasa huita (send off) na wengi wanapenda sana kuwaaga mabinti zao hasa mabinti wa kizazi cha siku hizi.

Wimbo
Kiongozi: *Gendelage wema Mikolina kulituwo fyala,*
pi kemela gendelage wema
kuliyuwo fyala pi kemela x 2

Kibwagizo: *gendelage wema kuliyuwo fyala*
pi kemela x 2

Tafsiri *Kiongozi: Tembea kwa adabu Mikolina anapokwita mama mkwe x 2*
Anapokuita mama mkwe tembea kwa adabu x 2

Watafitiwa wanasema kuwa watoto huimba wakiiga jinsi ambavyo nyimbo inavyoimbwa kwenye harusi wakati wa kumuaga binti anapokwenda kwa mumewe kuishi. Ambapo binti anatahadharishwa na kuaswa akawe mtii kwa wakwe zake. Pia kiburi hakifai na wakwe ndiyo wazazi atakao kuwa nao jirani zaidi. Ntarangwi (2014) akimtaja Charles Darwin anazungumzia juu ya binadamu kuwa uhalisia na ukweli hubaki palepale na hujikita katika mambo yaliyopo. Nadharia ya uhalisia katika jamii uhalisia huo upo katika jamii zote binti anapoolewa kwenda kuishi kiumeni huimbiwa nyimbo za kumuasa na makabila mengi hapa nchini hufanya hivyo.

4.2.8 Kudumisha Heshima

Heshima ni mafunzo ambayo yalitolewa kupitia nyimbo hususani nyimbo za watoto. Watafitiwa wanaeleza kuwa zipo nyimbo ambazo watoto waliziimba kwa ajili ya kuwaongoza kuwa na heshima kwa wakubwa hata wadogo nyimbo zifuatazo ni mfano wa mafunzo haya.

Wimbo
Kiongozi : *Lingu lingu msina baba, lingu x 3*
Kiitikio : *akalingulila x 3*
Kiongozi : *alingu*
Kiitikio : *akalingulia*

Tafsiri
Chungulia chungulia kama kuna baba chungulia
Akachungulia

Watafitiwa wanasema huimbwa watoto wakiwa wamekaa katika duara na wakati huo huo huwa wamepiga magoti. Wimbo huu huchezwa na jinsia zote. Wimbo unapendeza kama idadi ya watoto itagawanyika kwa mbili. Kusudi mtindo wanaoucheza uendane na wawili wawili. Watafitiwa wanasema kiongozi anapoanzisha wimbo wote huwa wanapigiza viganja vyao chini ya sakafu wakiwa wamepiga magoti. Kiongozi akisema a lingu wote hunyanyuka wakishika viuno vyao kwa mikono miwili huku wakitizamana wawili akirudia alingu hugeukiana na mtu aliyoko jirani kwa kumwacha wa kwanza.

Wamitila (2006) na Mulokozi (1996) wanasisitiza kuwa kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na ujumbe pia ifunze na kuadibu ili kuwaandaa watoto kwa maisha ya baadaye. Wimbo huo hapo juu unafundisha adabu watoto wasipende kuwachungulia wazazi wakiwa chumbani, au chooni na mahali popote. Nadharia iendanayo na wimbo huu ni nadharia ya uhalisia na nadharia ya Ualisia inayoangalia kuhusu dhima na dhamira pamoja na kazi mbalimbali, tabia kama hizi za watoto kutokuwa na nidhamu zipo katika jamii yetu, watoto wanapaswa kuelekezwa mazuri ni yapi na mabaya pia watoto wafunzwe heshima na adabu kwa lika zote.

Wimbo
Kiongozi: *Uwifu mwiko, mkomi gu mtela sangile vako*
wiyaule aaaa wiyaule aaaa u wiyaule

Uwifu mwiko mkomi gu mtela sangile
Vako wiyaule aaaa wiyaule aaaa wiyaule

Tafsiri:
Wivu ni mwiko. Jambo la muhimu hakikisha mmeo hakosi chakula pika ujikomboe.

Mazingira (1991) anasema nyimbo ni hazina ambayo husambaza mawazo juu ya maisha ya binadamu na maendeleo yake ambapo nyimbo hutoa mafunzo ya kuonya, kukosoa na kuadilisha jamii.

Watafitiwa wanaeleza kuwa wimbo huo huimbwa na watoto katika harakati za kumuonya mwali akawe na heshima na utii. Katika kuandaa chakula cha mumewe, Kuwa wivu haufai. Hivyo watoto wanapoigiza kumsindikiza bibi harusi ambaye anakuwa ameandamana na mumewe huimba nyimbo za kumtaka akawe na heshima, moja ya nyimbo ni kama huo. Wimbo huu unaendana na nadharia ya uhalisia inayoonyesha ukweli halisi wa maisha ya jamii. Hivyo katika jamii pia nyimbo za kuwaeleza watoto wawe na heshima zilikuwepo, na makabila mengi yanafanya hivyo. Katika tasnia ya muziki nyimbo za kufunza heshima zipo zinaimbwa na wasanii wetu ni vyema kuziendeleza hasa kwa watoto ambao ni hazina ya taifa letu la kesho.

4.3 Hitimisho

Utafiti huu umechunguza dhima katika nyimbo za asili za watoto katika kabila la Wahehe. Kutokana na uchambuzi wa data, utafiti umetoa matokeo yanayoonesha kwamba nyimbo za asili za watoto za kabila la Wahehe zina dhima mbalimbali kama vile: Dhima ya kuhimiza ya maadili mema, dhima ya kuonya, dhima ya kuelimisha,

dhima ya kuchapulisha kazi, dhima ya kudumisha mila na desturi, dhima ya mila, kuagana na wazazi na dhima Kudumisha heshima. Pia, mtafiti alibaini katika utafiti wake kuwa mbali na hizo dhima nyimbo huburudisha kwa lengo la kumpumzisha akili baada ya kazi nzito.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari kwa kila sura, kwa kifupi ili kuweka wazi kile kilichofanyika katika utafiti huu, sura hii inatoa mapendekezo yanayotokana na utafiti huu pamoja na maeneo yanayoweza kufanyia utafiti zaidi na wataalamu mbalimbali kuhusu nyimbo za watoto za asili za makabila.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu ulihusu dhima katika nyimbo za asili za watoto za kabila la wahehe. Kutokana na uchambuzi wa data, utafiti huu umetoa matokeo yanayoonesha kwamba nyimbo za asili za watoto za kabila la wahehe zina dhima mbalimbali kama vile: dhima ya kuelimisha, dhima ya kuonya, dhima ya kuchapulisha kazi, dhima ya mila na desturi, dhima ya uchawi, dhima ya kuagana na wazazi na dhima ya heshima.

Katika jamii ya wahehe nyimbo hizi zililenga kutoa mafunzo mbalimbali ni pamoja na kufunza umuhimu wa kazi, kuonya kuhusu wizi, ugomvi, ulevi na kuhimiza upendo na kufanya kazi. Pia nyimbo za kuburudisha watu wakichoka na kazi kwa lengo la kupumzisha akili baada ya kutoka kwenye kazi nzito walizozifanya.

5.3 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu kuchunguza dhima katika nyimbo za asili za watoto katika kabila la wahehe. Ili kutimiza lengo hili nadharia za uamilifu, uasilia na uhalisia zimetumika na kutupatia matokeo yaliyowasilishwa katika utafiti huu. Utafiti huu

umegawanyika katika sura tano ambazo ni: Sura ya kwanza inajumlisha, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu, malego ya mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya machapisho na marejeo, sehemu ya tatu inahusu mbinu na njia za utafiti. Sura ya nne inahusu uchambuzi wa data na sura ya tano Hitimisho, Muhtasari na Mapendekezo.

Mtafiti amechambua data ambazo zinahusiana na lengo mahususi la pili la utafiti huu, ambapo lengo hilo lililenga kuelezea nafasi ya dhamira za nyimbo za asili za watoto katika kabila la wahehe. Mtafiti amefanikiwa kubainisha dhamira 8. Dhamira ya Maadili mema, kuonya, kuelimisha, kuchapulisha kazi, mila na desturi, uchawi, kuagana na wazazi na dhamira ya heshima.

5.4 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu nyimbo za asili za watoto za kabila la wahehe imeonekana kuwa zina umuhimu mkubwa sana katika jamii mbalimbali kwani dhamira zake zina halisika katika jamii nyingi za Tanzania, hivyo mtafiti amependekeza yafuatayo:-

Ili tuweze kudumisha nyimbo za asili jamii haina budi kuipa sanaa hii ya nyimbo kipaumbele pia kuthamini mila na desturi za makabila mbalimbali ambazo hazijapitwa na wakati na chimbuko la nyimbo nyingi zinazoimbwa katika jamii ya watanzania.

Katika serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni iweke mkazo katika kuendeleza utamaduni wa asili wa Mtanzania. Mfano nyimbo za watoto za makabila

mbalimbali na nyimbo za makabila kwa ujumla kwa kuwa nyimbo nyingi za watoto huigwa kutoka nyimbo za wakubwa. Hii itasaidia watoto wetu kupenda nyimbo za asili badala ya kudumisha na kupenda nyimbo za nje kama vile reggae, bongo fleva na hip hop. Pamoja na kuiga tamaduni ngeni. Kwa hali halisi tamaduni za kigeni zimedumaza utamaduni wa mtanzania kama ilivyo dhihirishwa leo, na hasa pale ambapo mtafiti alipotembelea na kuwahoji watoto waliishio Kilolo kwani watoto wengi hawaelewi chochote kuhusiana na nyimbo za asili zaidi ya kuimba nyimbo mchanganyiko za kigeni toka makabila mengine (wahamiaji) nyimbo za kihehe wengi wao hawazijui.

Jukumu hili la kudumisha utamaduni wa mtanzania si jukumu la Wizara ya Elimu na serikali yake bali ni jukumu la watu wote wenye asili ya utanzania wazawa wa Tanzania yaani jukumu la wote, taasisi binafsi, pamoja na wadau mbalimbali wanaothamini utamaduni wa mwafrika.

Hivyo basi katika kudumisha na kuendeleza nyimbo za asili za watoto za makabila mbalimbali, ingefaa sana taasisi binafsi, pamoja na wadau mbalimbali kuandaa matamasha mbalimbali yatakayo jumuisha nyimbo za makabila mbalimbali na hivyo kufanya tamaduni za makabila yaliyopo kufahamika kiurahisi kwa ujumla wake ndani ya nchi na nje ya nchi.

MAREJEO

Balisidya, N. (1987). "Tanzu na Fani za Simulizi," *Mulika* na 19, TUKI: DSM.

Bond, S. (2002). "Culture and Feminine Leadership," in Women, *Power and the Academic from Rhiotic to Reality*, New York: Bargharin Books.

Cohen, L. (1980). *Research Methods in Education*, London: Routledge.

Enon, J. C. (1995). *Education research, statistics and measurement*, Kampala: Makerere University Press.

Finnegan, R. (1977). *Oral Poetry*, Nairobi: Cambridge University Press.

Finnergan, R. (1971). *Oral Literature in Africa.* London: Oxford University Press.

Gay, L. R. (1987). *Educational Research*: *Competence for Analysis and Application* (third edition), Ohio: Merrill Publishing Company.

Hussler, R. (1992). *Social Research Methods*, New York: West Publishing Company.

Kirumbi, P. S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*, Dar es Salaam: Shungwaya Publishers.

Kivenule, A. (2013). "Mila na Desturi za Kabila la Wahehe Mkoa wa Iringa," htt://adamkivenule.blogspot.2013.hub/com/blog.

Kombo, D. K. & Tomp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *An Introduction*, Nairobi: Puliness Publications.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology*: *Methods and Techniques* 2nd edition. New Delhi: New Age Internation Limited Publishers.

Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*, Ndanda: Benedictine Publishing Company.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*, Dar es Salaam: Ecumenical Gathering.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha,* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Msokile, M. (1981). "Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii iliyobadilika," Makala ya semina ya fasihi simulizi, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. (1989), "Tanzu na fasihi" *katika Mulika* namba 9, TUKI: Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1983). "Utafiti wa Faishi Simulizi," katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwakasaka, C. S. (1977). "The Oral Literarure of Banyakyusa," (M.A. Dissertation), University of Dar es Salaam.

Ndumbaro, E. (2012). "Makala ya Utafiti," Dar es Salaam: TUKI.

Nketia, J.H. (1963). *Drumming in Akan Communities*, London: Thomas Nelson and Sons Ltd.

Nkwera, F. (1981). *Tamrini za Fasihi Simulizi*, Peramiho: Ndanda Publishers.

Sengo, T.Y.S. (1978). "Kudidimizwa kwa Fasihi na Wakoloni." Taamuli ya Fasihi Dar es Salaam: TUKI.

Thonya, M. L. (1978). *Misingi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: Black Star Agencies.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Mombasa: Phoenix Publishers Ltd.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I

MUONGOZO WA HOJAJI KWA WAZEE (WATU WAZIMA)

1. Utangulizi

Mimi ni Mlambia Anna, ni Mwanchuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ninayefanya Shahada ya Udhamiri ya Sanaa katika Kiswahili (MA – Kiswahili). Nipo katika utafiti wa "**kuchunguza dhamira katika nyimbo za watoto za asili**" katika kabila la wahehe, wewe kama mdau unaombwa kutoa mchango wako wa mawazo na uzoefu katika kujibu maswali nitakayokuhoji. Napenda kukuhakikishia kuwa taarifa zote utakazonipatia zitatumika kwa utafiti na sio kwa nia nyingne yoyote ile.

2. Taarifa za awali za mhojiwa

   (i) Jinsia …….

   (ii) Umri ……..

   (iii)Kiwango cha elimu……

   (iv)Kata …….

   (v) Wilaya……..

   (vi)Lahaja ……..

3. (a) Kuna nyimbo unazozikumbuka mlizoimba utotoni za asili.

   _____

   _____

(b) Kama ndivyo kwenye swali (a) hapo juu, je unaweza kuzitaja nyimbo kama tano na kuziimba.

_____

_____

4. (a) Je nyimbo ulizozitaja ziliimbwa wakati gani

_____

_____

(b) Kwa uzoefu wako je nyimbo hizo zilizoimbwa zilikuwa na mafunzo au la?

_____

_____

(c) Kama ndiyo nini yalikuwa mafunzo ya nyimbo hizo.

_____

_____

5. Kwa uzoefu wako je unafikiri nyimbo za watoto za asili mlizoiimba wakati huo bado zipo?

_____

_____

KIAMBATISHO II

DODOSO KWA VIJANA (MIAKA CHINI 30)

1. **Utangulizi**

   Mimi ni Mlambia Anna, ni Mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ninafanya Shahada ya Udhamiri ya Sanaa katika Kiswahili (MA – Kiswahili) nipo katika utafiti wa "**kuchunguza dhamira katika nyimbo za watoto za asili**" katika kabila la wahehe. Wewe kama mdau unaombwa kutoa mchango wako wa mawazo na uzoefu katika kujibu maswali nitakayohoji. Napenda kukuhakikishia kuwa taarifa zote utakazonipatia zitatumika kwa utafiti na sio kwa nia nyingine yoyote ile.

2. Taarifa za awali za mhojiwa

   (i) Jinsia……

   (ii) Umri ……

   (iii) Kiwango cha elimu……

   (iv) Kata ……..

   (v) Wilaya……

   (vi) Lahaja…….

3. (a) Je kuna nyimbo unazozikumbuka mlizoimba za watoto za asili. Weka alama ya √ kwenye jibu lako

Ndiyo	
Hapana	

(b) Kama jibu ni ndiyo kwenye swali (a) hapo juu, taja walau nyimbo tano unazozikumbuka

_____

_____

4. (a) Je nyimbo ulizozitaja zinaimbwa wakati gani?

_____

_____

_____

(b) Kwa uzoefu wako je nyimbo hizo zilizoimbwa zilikuwa na mafunzo au la?

_____

_____

(c) Kama ndiyo hapo kwenye (b) nini yalikuwa mafunzo ya nyimbo hizo

_____

_____

5. Kwa uzoefu wako je unafikiri nyimbo za watoto za asili mlizoiimba wakati huo bado zipo

_____

_____

KIAMBATISHO III

MUONGOZO WA MAJADILIANO KWA VIKUNDI WATOTO

(FOCUS GROUP DISCUSSION GUIDE)

1. Utangulizi

Mimi ni Mlambia Anna, ni Mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ninafanya Shahada ya Udhamiri ya Sanaa katika Kiswahili (MA – Kiswahili) nipo katika utafiti wa "**kuchunguza dhamira katika nyimbo za watoto za asili**" katika kabila la wahehe. Wewe kama mdau unaombwa kutoa mchango wako wa mawazo na uzoefu katika kujibu maswali nitakayohoji. Napenda kukuhakikishia kuwa taarifa zote utakazonipatia zitatumika kwa utafiti na sio kwa nia nyingine yoyote ile.

2. (a) Kuna nyimbo unazozikumbuka ambazo huwa mnaziimba nyimbo za asili

_____

_____

(b) Kama ndiyo kwenye swali (a) hapo juu je unaweza kuzitaja kama nyimbo tano na kuziimba

_____

_____

3. (a) Je nyimbo ulizozitajwa mmekuwa mkiziimba wakati gani

_____

_____

(b) Je nyimbo hizo mlizoziimba zitakuwa na mafundisho au hapana.

_____

_____

(c) Kama zina mafundisho nitajie mafundishe au mafunzo unayoyafahamu.

_____

_____

(d) Je nyimbo mlizoziimba za watoto za asili wakati huu bado zipo

_____

_____

KIAMBATISHO IV

RATIBA YA UTAFITI

MUDA	**TUKIO**
FEBRUARI – APRILI, 2016	Uandaaji wa pendekezo la utafiti
APRILI – JUNI, 2016	Ukusanyaji wa data
JULAI – AGOSTI 2016	Uchambuzi na uchanganuzi wa data
AGOSTI – SEPTEMBA 2016	Uandaaji wa taarifa ya utafiti
AGOSTI – SEPTEMBA 2016	Uwasilishaji wa taarifa ya utafiti